**SAKATA** la mwanafunzi kuacha shule kutaka kuolewa laibua mapya

UKURASA 2



**RITA** yataja sababu sita za ndoa nyingi nchini kuvunjika

UKURASA 3


ama
AFYA NA MAZINGIRA
KWANINI MAMA ANAKATISHA KUNYONYESHA?
Wenyewe wasimulia ya moyoni, huku daktari bingwa akifunguka
WIKI YA MACHO
Mabingwa Muhimbili, CCBRT wamchambua mpofushaji namba mbili, presha ya macho

Siku tano za Naibu Waziri wa Maji Mbeya zenye neema kwa wakazi

•Atumia mguu kilomita kukagua •Pia wapo hawakuachwa salama

UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Machi 18, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580523

www.ippmedia.com

The Guardian digital   nipasheTZ   nipasheTZ   nipasheTZ   0745 700710


# Biashara binadamu yazidi kushika kasi

UKURASA 2



Wafanyabiashara wa nyanya, wakisubiri wateja katika Soko la Pugu, jijini Dar es Salaam jana, bidhaa hiyo imepanda bei kutoka 45,000/- kwa tenga moja hadi 70,000/-. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## CHADEMA yataja sababu za wateule BAWACHA kukaimu

UKURASA 2

## ATUHUMIWA KUUA MTOTO WA KAMBO KUMMWAGIA UJI WA MOTO

UKURASA 3

**MICHEZO** **GOMES AFUNGUKA ALIPOISHIKA MERREIKH** UK. 24

**MAONI, KATUNI UK. 6**



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akipata maelezo kuhusu utengenezaji wa Kadi Janja kutoka kwa Ofisa Ufundi wa kiwanda cha kutengenezea kadi hizo (Smart Card TLD), jijini Tanga jana. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigela. **PICHA: OMR**

# Biashara ya binadamu yashika kasi

**Na Beatrice Shayo**

KAMANDA wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, amesema kasi ya biashara ya usafirishaji binadamu nchini inazidi kiwango cha kimataifa, jambo linalotakiwa kudhibitiwa kulinda heshima ya Tanzania.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipofungua mkutano wa siku tatu uliowahusisha Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ustawi wa Jamii na Mahakama uliofadhiliwa na Tanzania Relief Initiatives (TRI) kwa ajili ya kujadiliana biashara ya usafirishaji wa binadamu.

Kamanda Mambosasa alisema Tanzania inakuwa ni mfano mbaya wa kuvunja rekodi katika kushiriki biashara hiyo haramu. Alisema biashara ya usafirishaji binadamu ni njia mpya ya utumwa wa kisasa ambayo imeenea duniani kote na inatishia maendeleo ya kisiasa na ukuaji wa kiuchumi, inatishia uwapo wa amani katika nchi na inadhoofisha utu kwa binadamu.

Alisema baadhi ya watu wasio waaminifu hutumia vibaya taratibu za kijadi za kusaidia kulea watoto, akibainisha kuwa watoto maskini hukabidhiwa na kutunzwa na ndugu wenye uwezo bora wa maisha au wanajamii wanaoheshimiwa na hivyo kutumia watoto hao kufanya kazi za kulazimishwa.

Alisema unyonyaji wa wasichana wadogo katika kazi za ndani na utumikishwaji katika ukahaba, unaendelea kuwa tatizo kubwa la biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu nchini. "Wanandugu hushiriki na wapo marafiki na wengine ni madalali kwa kudanganya kuwa watoto wanapotoka kuja mjini kuna maisha mazuri zaidi na ndugu wengine wanapokuwa hawana uwezo na kuwaachia watu wengine kuwalelea watoto wao," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema watazitumia siku tatu kujifunza, kujengeana uwezo, kubadilishana uzoefu na kuweka mikakati ya pamoja ya kuhakikisha biashara hiyo haramu ya kusafirisha binadamu kwa Tanzania na kwa Jiji la Dar es Salaam ambapo hutumika kuingia na kutokea inapungua.

Alisema biashara hiyo ina madhara makubwa na wengi wao wanaosafirishwa ni vijana wenye umri mdogo ikiwamo watoto wa kike ambao hupelekwa kwa madhumuni ya kutumikishwa kazi za ndani na kingono.

Alisema taifa linavyowapoteza vijana wadogo wanapokwenda kutumikishwa, mwisho wake ni kupoteza nguvu kazi ya taifa na kushiriki katika kumong'onyoa maadili.

Alisema Tanzania ilitunga sheria mbalimbali ili kuunga juhudi za kimataifa ili kupambana na tatizo hilo ikiwamo Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu na Usafirishaji ya Binadamu ya Mwaka 2008 na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009.

Mkurugenzi wa Shirika la TRI, Edwin Mugambila, alisema biashara ya usafirishaji wa binadamu ni biashara inayokua kwa kasi duniani na kwa mujibu wa ripoti za hivi karibuni, Tanzania ni nchi ya tatu kwa tishio ya biashara hiyo duniani.

Alisema biashara hiyo inatengeneza fedha nyingi kwa mujibu wa takwimu, hivyo inaonyesha ni kwa namna gani ni tishio.

Alisema biashara hiyo haitambui mipaka hivyo inakuwa ni ngumu kwa nchi moja ama taasisi moja kupambana nayo.

# CHADEMA yatoa sababu wagombea kukaimu

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimefafanua sababu za wagombea wa nafasi za uongozi katika Baraza la Wanawake la chama hicho (BAWACHA) kukaimishwa nafasi hizo badala ya kupewa uongozi kamili.

Juzi, chama hicho kilitangaza wagombea 29 waliojitokeza kuwania nafasi mbalimbali ziliozoachwa wazi baada ya kufukuzwa waliokuwa makada wa chama hicho.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Makamu Mwenyekiti wa BAWACHA Zanzibar, Sharifa Suleiman, nafasi hizo zitakaimishwa hadi hapo rufani zilizokatwa na Halima Mdee (aliyekuwa Mwenyikiti wa Baraza hilo) na wenzake zitakaposikilizwa.

"Ni kwa sababu wale wengine (Halima Mdee na wenzake) wamekata rufaa (rufani) ambayo inatarajiwa kusikilizwa na Baraza Kuu la Chama kwa hiyo bado wana haki," alisema Sharifa.

Novemba 24, mwaka jana, makada 20 wakiongozwa na Halima Mdee, aliyekuwa Mwenyekiti wa BAWACHA, walikwenda bungeni jijini Dodoma kuapishwa ili kuchukua nafasi 19 za ubunge wa viti maalum kinyume cha msimamo wa chama hicho kilichopinga matokeo ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 na kukubaliana kutokubali nafasi zozote zilizotokana na uchaguzi huo.

Mbali na Mdee, wengine waliofukuzwa ni aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Baraza Tanzania Bara, Hawa Mwaifunga, Katibu Mkuu Grace Tendega, Naibu Katibu Mkuu Bara Jesca Kishoa, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar Asia Mohamed, Katibu Mwenezi Agnesta Lambert, Katibu Mkuu wa Baraza la Vijana Nusrat Hanje na aliyekuwa Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Serengeti, Esther Matiko.

Wengine ni Cecilia Pareso, Tunza Malapa, Ester Bulaya, Felister Njau, Sophia Mwakagenda, Ngahenjwa Kaboyoka, Kunti Majala, Anatropia Theonest, Conchesta Rwamlaza, Salome Makamba na Stella Fiao.

Tayari wabunge hao wameshakata rufani ndani ya chama kupinga uamuzi wa kufukuzwa uanachama tangu Januari, mwaka huu, ingawa mpaka sasa haijajulikana tarehe rasmi ya kusikilizwa kwa rufani hizo.

# Sakata mwanafunzi laibua mambo mapya

**Na Francis Godwin,** IRINGA

SAKATA la mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Mtwivila, Manispaa ya Iringa, kumwandikia barua mkuu wa shule ili aache shule na kwenda kuolewa limechukua sura mpya baada ya serikali ya wilaya kutangaza msako wa nyumba kwa nyumba kwa wanaojihusisha na mapenzi na wanafunzi.

Akizungumza jana na Nipashe, Katibu Tawala Wilaya ya Iringa, Sthomen Kyando, alisema wamewaagiza waratibu elimu kata, maofisa watendaji kata na vijiji na mitaa kuanza msako wa kuwapata wanafunzi ambao hawajaripoti kidato cha kwanza.

Pia msako huo utahusisha wanaojihusisha na uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi.

"Mbali na suala hili la mwanafunzi wa Mtwivila ambaye kaandika barua kwa Mkuu wa Shule kutaka kuacha shule kwenda kuolewa, viongozi wa wilaya tulianza mapema kuwafuatilia wanafunzi waliofaulu kwenda sekondari na hawajaripoti. "Tayari tumeanza kuchukua hatua kali ikiwa ni pamoja na kuwafikisha wazazi mahakamani na hadi sasa wazazi 10 wamefikishwa Mahakama ya Mwanzo Kiponzero," alisema. Katibu Tawala huyo alisema wazazi hao ni kati ya wazazi wa wanafunzi 27 wanaosakwa kwa kutowapeleka watoto shuleni na kwamba lengo ni kujua sababu za kutoripoti.

Naye Ofisa Elimu Sekondari Manispaa ya Iringa, Tupe Kayinga, alisema wanaendelea kumfuatilia mwanafunzi aliyeandika barua ili kumrejesha shuleni.

Pia alisema mkuu wa shule hiyo aliripoti suala la mwanafunzi aliyeandika barua ofisi ya elimu manispaa.

**MWINGINE AOZESHWA**

katika hatua nyingine, mbali na mwanafunzi huyo, Kayinga alisema ofisi yake inaendelea kumfuatilia mmoja wa wazazi mjini hapa ambaye alimruhusu mtoto wake kwenda jijini Dodoma kutafutiwa mume wa kumuoa badala ya kumpeleka shuleni.

Alisema kwa kushirikiana na ofisi ya ustawi wa jamii pamoja na dawati la polisi, ili kuwabana wazazi na watoto ambao hawajaripoti shule pamoja na kufaulu na kuchaguliwa kwenda sekondari.

Manispaa ya Iringa, alisema wanafunzi 106 ambao hawajaripoti shule pamoja na kufaulu na kuchaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari.

Meya wa Manispaa ya Iringa, Ibrahim Ngwada, alisema lengo la kujenga shule za sekondari ni kuwezesha watoto wote wanakwenda shuleni kinyume cha malengo ya serikali kuona watoto wanatumikishwa kazi za ndani ama kuozwa kinyume cha sheria.

Aidha, aliagiza walimu kutowafukuza wanafunzi wanao kwenda shule bila sare za shule.

**HABARI KITAIFA**

# Atuhumiwa kumuua mtoto wa kambo kummwagia uji wa moto

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

JESHI la Polisi mkoani Kagera, linamshikilia Leticia Protazi (42), mkazi wa Kijiji cha Kyamyorwa, wilayani Muleba kwa tuhuma za kusababisha kifo cha mtoto wake wa kambo Arian Adelius (2), kwa kummwagia uji wa moto.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kamanda wa Polisi mkoani humo, Revocatus Malimi, alisema Machi 12, mwaka huu, majira 3:00 asubuhi, polisi ilipokea taarifa za tukio hilo.

Kamanda Malimi alisema sababu ya kifo hicho ni ugomvi ulioibuka baina ya mtuhumiwa na mama mzazi wa marehemu huyo, Hapinnes Fidel, uliotokea kwenye kikao cha kutambulishwa kwa mtuhumiwa kwenye familia ya mume wao kuwa mke mdogo.

"Uchunguzi wa polisi umebaini kuwa siku ya tukio hilo kulikuwa na kikao cha familia kilichokuwa kimeandaliwa na mume wa mtuhumiwa nyumbani kwa wazazi wake cha kumtambulisha mke wake wa pili ambacho pia kilihudhuriwa na mke mkubwa," alisema Malimi.

Alisema katika kikao hicho, mke mkubwa alikuwa ameambatana na mtoto wake huyo (marehemu).

Alisema wakati kikao kikiendelea ndipo ugomvi ulipotokea baina ya wanawake hao na mke mkubwa baada ya kuona mtuhumiwa amekwenda kuchukua sufuria ya uji wa moto ili ammwagie, alikimbia na kumuacha mtoto wake.

"Mtuhumiwa wetu alichukua sufuria lililokuwa pembeni kwa lengo la kummwagia mke mwenzie ambaye ni mke mkubwa na mama mzazi wa mtoto, lakini aliwahi kukimbia ndipo mtuhumiwa akaamua kummwagia mtoto," alisema Malimi.

Kamanda alifafanua kuwa uji huo alimwagiliwa mtoto sehemu za tumboni na kukimbizwa kituo cha afya cha Kushanje, kwa kuwa hali yake ilikuwa mbaya.

# Sababu sita ndoa nyingi kuvunjika

**Na Mary Geofrey**

WAKATI takwimu za Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) zikionyesha talaka 511 zilisajiliwa mwaka jana huku mkoa wa Dar es Salaam ukiongoza kwa talaka 247, viongozi wa dini wamebainisha sababu sita zinazochangia ikiwamo kuyumba kwa uchumi.

Sababu nyingine ni ndoa nyingi kutoanzia kwa wazazi na pindi unapotokea mgogoro kati ya wanandoa hao, huishia kumalizana kwa kuachana bila kutafuta suluhu.

Amiri Mkuu, Baraza Kuu la Jumuiya ya Taasisi za Kiislamu, Sheikh Mussa Kundecha, aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam katika semina iliyojumuiya RITA na viongozi wa dini ili kujadili masuala mbalimbali ya utendaji kazi na ushirikiano wao.

Pamoja na mambo mengine, walijadiliana kuhusu mabadiliko ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inayotakiwa kufanyiwa marekebisho, kukithiri kwa talaka na elimu kuhusu mirathi.

Alisema sababu ya uchumi inatokea wakati ambao mwanamume na mwanamke waliamua kuoana kwa sababu ya mali na uchumi ukiyumba, ndoa hiyo huvunjika.

"Lipo tatizo la wanaume kutoa talaka kwa sababu ya ugumu wa maisha. Anaanza kutoa visingizio vingine vya kutaka kuachana lakini ukweli unakuwa na hali ya uchumi.

"Ndoa chache sana siku hizi zinatokana na chanzo cha wazazi. Zinazoanza na wazazi, linapotokea tatizo, wanarudi nyumbani wanasuluhishwa wanaendelea kuwa pamoja lakini wengine wanakutana, kufunga ndoa na kuachana bila wazazi kushirikishwa," alisema Sheikh Kundecha.

Alisema sababu nyingine ni kukua kwa utandawazi kunakosababisha watu kufahamu mambo mengi huchangia ndoa nyingi kuvunjika.

"Wanaume walizoea kuwa wao ndiyo wanakuwa wanasikilizwa, wanafanya uamuzi bila kuingiliwa lakini sasa utandawazi umekua, wanawake wanafahamu haki zao," alisema Sheikh Kundecha.

Alisema wapo watu wanaoana kwa sababu ya mapenzi peke yake, ikitokea yameshuka, wawili hao hutengana kwa kuwa wamekosa kinachowaunganisha.

Mchungaji wa Kanisa la Waadventista Wasabato Kusini mwa Tanzania, Elisante Mshama, alisema sababu nyingine ni mila na tamaduni zinazokinzana na utandawazi.

Alisema mila na desturi za miaka ya nyuma zilikuwa zikiwaweka pamoja wanandoa, lakini kwa sasa zinaonekana kama kukandamiza upande mmoja.

Alifafanua kuwa licha ya kuwa ndoa ni muunganiko wa hiari wa watu wawili, kumekuwapo na ongezeko la wanandoa kuachana bila kufuata taratibu za mabaraza ya dini.

Alisema wanandoa wamekuwa wakitofautiana na kukimbilia mahakamani bila kushirikisha mabaraza ya dini na viongozi, hali inayofanya ndoa nyingi kuvunjika bila kupatiwa suluhu.



Waziri Waziri wa Katiba na Sheria. Dk. Mwigulu Nchemba.

Kiongozi huyo wa kanisa alisema wanajitahidi kutoa elimu ya ndoa, lakini wanandoa wenyewe wamekuwa wakaidi kwa kufikisha migogoro mahakamani bila kupitia kwa viongozi wa dini.

"Tunajitahidi sana kufungisha ndoa na kuzikaza kabisa, lakini masuala hayo yanafikishwa ngazi ya mahakama mapema na kusikilizwa haraka na kwa muda mfupi na hati ya talaka inatoka haraka.

"Hata kupata nakala ya hukumu kwa wakati ni changamoto, hivyo wengi wanashindwa kukata rufani," alisema Mchungaji Mshama.

Awali, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba, aliwataka viongozi hao wa dini kusimamia na kutoa elimu ya ndoa kutokana na kuwapo kwa ongezeko la ndoa nyingi kuvunjika nchini.

"Mashauri ya kuomba talaka kwa Dar es Salaam peke yake ni 1,500 na kuendelea, ni nyingi sana. Sijui mnavyofungisha ndoa kuna sehemu gani mnalegeza ndiyo maana zinaongoza kuvunjika. Angalieni namna ya kukaza," alisema Nchemba.

Talaka 511 zilisajiliwa mwaka jana likiwa ni ongezeko la talaka 68 kulinganishwa na talaka 442 zilizosajiliwa mwaka 2019.

Company No. 137003740

**THE COMPANIES ACT, 2002**

**COMPANY LIMITED BY SHARES**

**MEMBERS' SPECIAL RESOLUTION OF LOANS TECHNOLOGY TANZANIA LIMITED**

At an Extra Ordinary General Meeting of the Shareholders of the Company duly convened and held on 15th the day of March, 2021 at the registered office of the company.

**RESOLUTIONS:**

The following resolutions were duly passed pursuant to section 400 (3) of the Companies Act:

I. The Company be struck off the Register of Companies and the Board of Directors of the Company lodge an application to the Registrar of Companies, under the provisions of Section 400 (3) of the Companies Act, 2002 to strike off the name of the Company from the Register of Companies.

II. **FURTHER RESOLVED:** The Board of Directors of the Company is hereby authorized to do all such matters, deeds and things as may be required under the provisions of the Companies Act, 2002 and the rules made there under to ensure that the striking off of the Company is completed in compliance with the law.

**Signatures:**

Name: **IGOR ROGACHEV**
**Chairman**

Name: **JOVIN JONATHAN TIBENDA**
**Company Secretary**

Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Sky Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O. Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania

Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

**TANGAZO LA MINADA YA HADHARA**

**VICTORIA FINANCE PLC** INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA WA WATANZANIA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | AINA NA SEHEMU YA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ABDULRAHMAN A RAJABU | NYUMBA | HATI YA MAUZIANO – UBUNGO MSEWE | J&J RECOVERIES | 28-03-2021 |
| 2 | AMINA SAIDI JUMA | NYUMBA | HATI YA MAUZIANO – MANZESE | J&J RECOVERIES LTD | 29-03-2021 |
| 3 | EVELINE RODES MMARI | NYUMBA | HATI YA MAUZIANO – CHANIKA | J&J RECOVERIES LTD | 30-03-2021 |
| 4 | MAIMUNA A. MPANDA | NYUMBA | HATI YA MAUZIANO – KIMARA "B" | J&J RECOVERIES LTD | 19-04-2021 |
| 5 | IPUNGU MARTHA ADAM | NYUMBA | HATI YA MAUZIANO – CHANIKA | J&J RECOVERIES LTD | 31-03-2021 |
| 6 | STELLA MARTIN HIZA | NYUMBA | HATI YA MAUZIANO – BUNJU | J&J RECOVERIES LTD | 21-04-2021 |
| 7 | BEN PERVEMENT ENTERPRISES | NYUMBA | HATI YA MAUZIANO – MBWENI | J&J RECOVERIES LTD | 14-04-2021 |
| 8 | BEN PERVEMENT ENTERPRISES | NYUMBA | HATI YA MAUZIANO – KINYEREZI | J&J RECOVERIES LTD | 16-04-2021 |
| 9 | GWANTWA CONTRACTORS | GARI | TOYOTA LANDCRUISER PRADO T 832 CPL | GSP AUCTION MART | 23-03-2021 |
| 10 | GASTO PIUS TOWO | GARI | SUBARU IMPREZA T234 DKN | UMOJA PROFESSIONALS | 22-03-2021 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika ofisi za wakuu wa wilaya wanaohusika.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Taratibu na gharama za kubadili hati miliki kadi ya gari ni juu ya mnunuzi.

## Huduma maji vijijini kufikia asilimia 88

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MAMLAKA ya Maji Vijijini (RUWASA), Mkoa wa Iringa imeendelea kuimarisha usimamizi wa sekta ya maji, ili kuhakikisha inawafikia wananchi wote waliozungukwa na vyanzo vya maji na kupata huduma ya majisafi na salama kwa asilimia 86, mwaka 2025.


Meneja wa RUWASA mkoani Iringa, Joyce Bahati, alisema hayo juzi kwa wajumbe wa kamati ya siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani humo, ikiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Dk. Abel Nyamahanga, wakati wa ukaguzi wa miradi ya maji katika Wilaya ya Mufindi.

Alisema RUWASA inajitahidi kwenda na kasi kutekeleza mpango wa matumizi ya maji kwa wananchi ili kuendana na sera ya wizara pamoja na ilani ya CCM katika kuwasogezea huduma za maji wananchi.

Hadi sasa wamefanikiwa kufikia lengo la kutekeleza miradi 25 kati ya 38 ambayo mingine imekamilika.

Aliwataka wananchi kuendelea kutunza vyanzo vya maji ili visiharibiwe wala kuchafuliwa kwa kuwa ndio tegemezi kwa matumizi sahihi na kuwafikia watumiaji majisafi na salama.

Mwenyekiti wa CCM mkoani Iringa, Dk. Nyamahanga, alimpongeza Meneja wa RUWASA mkoani humo kwa kuhakikisha miradi yote ya maji inafanya kazi na kuwafikia wananchi.




Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile (kushoto), akikabidhi hati ya kiwanja kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Posta Afrika, Yonus Djibril, kwa ajili ya eneo linapojengwa jengo la ofisi za makao makuu ya Posta, jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# BoT yaonya VICOBA visivyosajiliwa

**Na Salome Kitomari**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imesema kikundi chochote cha huduma ndogo za fedha kitakachoendelea na shughuli zake bila usajili kitachukuliwa hatua kali, ikiwamo kufungwa au faini.

Meneja wa Huduma Ndogo za Fedha na Maduka ya Kubadilisha Fedha, Victor Tarimu, alisema jana kuwa mwisho wa usajili ni Aprili 30, mwaka huu, na tayari maofisa maendeleo ya jamii wameshapatiwa elimu na usajili umeanza.

"Tunashauri vikundi vyote vichangamkie fursa hii ya usajili kwa mujibu wa sheria kwa kuwa serikali ina malengo mazuri kurasimisha ili viendelee kutoka mchango mkubwa kwa wanachama wake na kumkomboa mwananchi wa kawaida kutoka kwenye umaskini hadi hali nzuri zaidi," alibainisha.

Kwa mujibu wa Tarimu, faida za usajili wa vikundi vidogo vya huduma ndogo za fedha kuwa ni pamoja na kunufaika na mikopo ya uwezeshwaji inayotolewa na serikali.

Aidha, alisema serikali ina mifuko mingi ya kusaidia wananchi, hivyo ni rahisi kupata misaada kutoka kwenye taasisi za serikali kwa kuwa vikundi hivyo ni muhimu kuwatoa watu katika umaskini na kwenda kwenye hali nzuri zaidi.

Vikundi vikisajiliwa, alisema vitakuwa na nguvu ya kisheria, hivyo ni rahisi kupata mikopo kwenye benki na ufadhili kwa sababu vinakuwa ni vikundi ambavyo vimeshatambulika rasmi.

"Sheria imeweka bayana kuwa ni lazima vikundi vyote vipate elimu ya fedha kwa sabau vingi havifanyi vizuri kwa sababu hawana elimu ya fedha, watoa huduma katika vikundi na wanaotumia huduma hawana elimu wanafanya miamala ya kifedha bila uelewa na kushindwa kupata faida inayotakiwa," alisema Tarimu.

Pia BoT ilisisitiza kuwa usajili ni bure kwa kuwa gharama za usajili zimebebwa na serikali na wanachopaswa ni kwenda serikali za mitaa kwa ajili ya kupata utambulisho na baadaye halmashauri ambapo kuna Ofisa Maendeleo ya Jamii.

Tarimu alisema kumekuwa na upotoshaji uliozua taharuki kuwa serikali itachota fedha kwenye vikundi hivyo kiasi cha baadhi ya vikundi kuvunjwa, jambo ambalo siyo kweli kwa kuwa lengo la serikali ni kurasimisha ili viweze kusaidiwa vinatambulika mchango vinaotoa katika jamii.

"Takribani asilimia 70 ya wananchi wa kipato cha chini wanapata huduma za kifedha kwenye vikundi, serikali iliona ni sekta inayohitaji kuendelezwa, kusaidiwa ili itoe mchango zaidi ili kusaidia wananchi kutoka katika umaskini kwenda hali nzuri zaidi, serikali haina mpango wa kuweka tozo au kodi kwenye vikundi," alifafanua meneja huyo.

Kwa mujibu wa Tarimu, VICOBA vimesaidia ujumuishi wa fedha ambayo ina mchango mkubwa katika maendeleo ya taifa, na ndiyo maana serikali imekuja na utaratibu wa kusajili.

Alisema kitakachofuatiliwa ni biashara ya fedha ya kukopesha na kurudisha na kwamba atakayepata mkopo ni jukumu lake na kikundi, na kwamba wakisajiliwa watapata mikopo ambayo itasaidia kukuza mikopo na kupata mikopo mikubwa zaidi.

Kwa mujibu wa kanuni ya 4 hadi 7 mwaka 2019 watoa huduma ndogo za fedha, VICOBA vinatakiwa kufanya mkutano wa awali, kuwa na kamati ya mpito na majukumu yake na kikao cha uanzishaji na majukumu yake.

Kanuni ya 8 hadi 17 ni maombi ya usajili yakiambatana na nakala ya katiba yenye sahihi za wanachama, nakala za mihtasari ya mkutano wa uanzishaji, maazimio ya wanachama kuanzisha kikundi.

Vinatakiwa kuwa na mapendekezo ya muundo wa kikundi, uthibitisho wa malipo ya michango ya awali, barua ya mamlaka ya kata au kijiji, na jina la kikundi lijumuishe maneno 'kikundi cha huduma ndogo za fedha cha kijamii' na baada ya kukamilisha wanakikundi watatakiwa kufanya kikoa cha kwanza ndani ya mwezi mmoja.

# Tanzania, China zaahidi kukuza ushirikiano

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, jana alikutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa China nchini, Wang Ke, katika ofisi za wizara jijini Dodoma.

Taarifa ya wizara ilisema wawili hao walijadili masuala mbalimbali yanayolenga kudumisha ushirikiano na uhusiano wa kidiplomasia na biashara.

Pia wamejadili kuhusu ufuatiliaji wa maendeleo ya miradi na programu mbalimbali zinazotekelezwa kwa ushirikiano wa Tanzania na China ili kuhakikisha zinaleta tija kwa manufaa ya pande zote mbili," ilisema taafia hiyo.

Balozi Ibuge, kwa mujibu wa taarifa hiyo, alisema kuwapo kwa uhusiano mzuri wa kidiplomasia baina ya Tanzania na China, kumechagiza kwa kiasi kikubwa kukua kwa biashara, utalii na uwekezaji baina ya nchi hizo.

Alisema urafiki na undugu kati ya mataifa haya mawili unapaswa kulindwa, kudumisha na kuendelezwa siku zote na katika hali yoyote.

"China kwa muda mrefu imekuwa ikichangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya taifa letu kupitia sekta mbalimbali kama vile ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji na mawasiliano kama vile reli na barabara, hivyo wizara na serikali kwa ujumla inathamini na kulinda undugu huu wa kihistoria," alisema.

Naye Balozi Wang alishukuru kwa ushirikiano ambao amekuwa akiendelea kuupata kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na serikali kwa ujumla katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku.

Balozi Wang aliahidi kuendelea kutoa ushirikiano ili kuhakikisha serikali za nchi hizo mbili na watu wake wananufaika kotokana na uhusiano mzuri wa kidiplomasia uliopo.

# Miradi 30 ya uwekezaji yaibuliwa maeneo ya SGR

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Dk. Maduhu Kazi, amesema miradi ya uwekezaji 30, imeibuliwa kwenye maeneo ambayo reli ya kisasa (SGR) imepita na kuwataka wananchi kuchangamkia fursa hiyo.

Aidha, baadhi ya fursa za miradi hiyo ya uwekezaji iliyoibuliwa ni kilimo, hoteli, viwanda, migahawa na uwekezaji katika taasisi za kifedha.

Dk. Kazi aliyasema hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika kikao cha kujadili fursa zilizopo katika mapito ya SGR, kilichohudhuriwa pia na Mkurugenzi wa Shirika la Reli (TRC), Masanja Kadogosa.

Alisema tangu Septemba mwaka jana TIC kwa kushirikina na taasisi mbalimbali za serikali wamekuwa na mchakato wa kutafuta na kuibua fursa zilizopo kwenye mradi wa SGR.

"Miradi hii ni ile ambayo itaongeza shughuli za usafirishaji katika njia hii ya reli na siyo kutegemea abiria pekee yao, hivyo basi miradi kama ya kilimo itatoa malighafi nyingi ambazo zitahitaji kusafirishwa kutoka sehemu moja kwenda nyingine," alisema Dk. Kazi.

Alisema kati ya miradi 30, ni miradi 14 ambayo ndiyo imeshakamilika kwa ajili ya kufanyiwa uwekezaji, hivyo wameona ni muhimu sasa kukutana na sekta binafsi ili kuiuza.

"Leo hii katika kikao hiki pia tumewaita wenzetu wa sekta binafsi ambao wametupa mawazo mazuri sana katika miradi hii ambayo tumeiibua na baadaye wataalamu wataiweka vizuri na tutaandaa kitabu ambacho kitatumia kuiuza kwa wawekezaji pamoja na kwenye tovuti yetu," alisema.

Vilevile, alisema wameona ipo haja kwa miradi ambayo ipo chini ya taasisi za serikali kuanza kabla ya ile inayohitaji wawekezaji.

"Miradi kama ya upimaji wa ardhi, uwekaji wa nishati ya umeme pamoja na maji na miundombinu mingine ambayo ipo chini ya taasisi za serikali inatakiwa kuanza haraka kabla ya ile ya viwanda," alisema.

Naye Kadogosa, alisema lengo la kikao hicho ni kukutana na wadau mbalimbali ili kuhakikisha wanapata wawekezaji katika maeneo ambayo reli ya SGR inapita.

"Hili ni agizo la mweshimiwa Rais Magufuli, alilolitoa alipotembelea mradi huu wa ujenzi wa reli ya kisasa na kututaka kuhakikisha kuwa katika maeneo ambayo reli imepita kunakuwapo na shughuli za uwekezaji ili kuchochea utendaji wa shirika," alisema Kadogosa.

Mwakilishi kutoka Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Kenned Rwehumbiza, alisema wameshiriki katika kikao hicho ili kuzitambua fursa za uwekezaji zilizopo katika mradi wa reli ya kisasa SGR na kuzifikisha kwa wananchi.

"Lakini kazi yetu kubwa ni kuangalia namna gani tunaweza kuzikana hizi fursa na kuzipeleka kwa wananchi ili waweze kuzifanyia kazi kwani tunaelezwa kuwa kuanzia Agosti mosi mwaka huu safari za Dar- Moro zitaanza," alisema.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa wa Benki ya CRDB, Gerald Kamugisha, alisema kupitia fursa zilizopo kwenye mradi wa SGR wao watashiriki katika kutoa mikopo kwa watu watakaokuwa tayari kuwekeza katika shughuli mbalimbali.



Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Richard Kayombo (kushoto), akisisitiza umuhimu wa kutunza kumbukumbu za biashara kwa wafanyabiashara wa eneo la Kipunguni B maarufu kama Moshi Bar, wakati wa kampeni ya Mlango kwa Mlango yenye lengo la kutoa elimu ya kodi inayoendelea, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Samia akunwa na miradi maendeleo

**Na Maulid Mmbaga**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amepongeza jitihada zinazofanyika katika kutekeleza miradi ya kimaendeleo mkoani Tanga ikiwamo ya viwanda na bandari ambayo itachochea ongezeko la pato la taifa.

Samia aliyasema hayo jana wakati akihutubia wananchi katika siku ya tatu ya ziara yake humo baada ya kutembelea miradi mbalimbali ya kimaendeleo kikiwamo kiwanda cha kutengeneza kadi janja.

Alisema Bandari ya Tanga kwa sasa ni ya pili kwa upakiaji na upokeaji wa mafuta nchini baada ya ile ya Dar es Salaam na itasaidia katika kusambaza mafuta ukanda wa kaskazini na nje ya nchi.

"Tanga kuna mambo makubwa sana na kama mlivyomsikia mkuu wa mkoa anasema bado kuna viwanda vingine vinane vinakuja na ukishavikamilisha na ukaniita nitakuja. Mimi katika viwanda sina masihara kwani najua hivyo ndivyo mkombozi wa ajira kwa vijana wetu na kodi ipo pale na vinachangia pato la nchi yetu," alisema.

Samia pia alisema kupitia Bandari ya Tanga kuna eneo kubwa litakalotumika kuhifadhia mafuta ya nchi na yale yatakayokwenda nchi za jirani.

Naye Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Leonard Chamuriho, alisema ujenzi wa Bandari ya Tanga utasaidia kupunguza msongamano wa meli na mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam. Pia alisema itasaidia kupunguza gharama ya uagizaji wa bidhaa nchi jirani kwa kuwa zitapatikana eneo hilo.

Waziri Chamuhiro alisema awamu ya pili ya uboreshaji wa bandari hiyo, itasaidia kuwezesha meli kubwa kuingia kutokana na kina cha bandari hiyo kuongezeka urefu kwenda chini kutoka mita nne hadi 15.

"Hiyo ina maana kwamba kwa sasa maji yakiwa yamekupwa meli kubwa ya tani 35,000 inaweza kuingia na wakati maji yamejaa inaweza kuingia yenye uzito wa tani 65,000 na kwa kulithibitisha hilo hata juzi iliingia meli ya mafuta yenye uzito wa tani 55,000," alisema Chamuriho.

Aliongeza uwekezaji huo mkubwa uliofanyika katika bandari hiyo umeshaanza kuzaa matunda na kwa sasa wanaendelea na utaratibu wa ununuzi wa vifaa vya upakiaji ili bandari hiyo iwe kuu kwa kanda ya kaskazini kwa kuchukua shehena za mikoa ya ukanda huo na hata za nje ya nchi kama Rwanda, Burundi na Congo.

Pia alisema mafanikio mengine waliyoyafikia katika utekelezaji wa mpango mkakati wa bandari hiyo ni kukamilika kwa mtambo wa kupimia viwango vya ubora wa mafuta ambao utasaidia kujua ubora wa malighafi kabla ya kwenda kutumika.

Alisema katika bandari hiyo kuna vituo viwili vya kupakia mafuta, cha kwanza kitakuwa cha malori ambayo yatachukua malighafi na kuisambaza mikoa yote ya jirani na cha pili kitakuwa na uwezo wa kupatia takribani mabehewa 20 ya mafuta kwa wakati mmoja.

# JKCI yashauriwa kwenda mikoani

**Na Christina Mwakangale**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, imeishauri Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) kuwa na vituo vya huduma za kibingwa za moyo katika hospitali za kanda nchini.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mwenyekiti wa kamati hiyo, Stanslaus Nyongo, baada ya kamati kufanya ziara JKCI, jijini Dar es Salaam.

Alisema kutokana na kituo hicho kuwapo Dar es Salaam pekee, licha ya hospitali za mikoa nchini kutoa huduma za matibabu ya moyo, kuna uhaba wa wataalamu bingwa waliobobea kwenye tiba hiyo.

"Kituo hiki kipo Dar es Salaam kuna wananchi wengine mikoani wanahitaji huduma. Vilevile wako ambao wana magonjwa ya moyo ila hawajui na watoto pia wanazaliwa na tatizo na haijulikani.

Sasa taasisi hii itoe mafunzo maalumu kwa madaktari kuanzia vituo vya afya, zahanati za vijijini kuwatambua haraka ili wafike huku kwa ajili ya matibabu," alisema Nyongo. Kadhalika, Nyongo aliongeza kuwa kamati imeitaka Wizara ya Afya, kuajiri wataalamu wa afya katika taasisi hiyo ili kukabiliana na uhaba wa wataalamu.

Pia alisema kamati imeridhika na huduma zinazotolewa na taasisi hiyo pamoja na uwekezaji wa vifaa tiba unaofanya huduma za kibingwa kutolewa nchini ikiwamo nchi jirani.

"Zamani ilikuwa matibabu kama haya ilikuwa nje ya nchi, huduma hii inahitajika kwa Watanzania na hata nchi jirani, ili kujiongezea kipato wanaweza kutoa huduma kupitia bima za kimataifa kwa wagonjwa wanaotoka nje ya nchi," alisema


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Mahakama ya Mwanzo ya SINZA**

**Wilaya ya KINONDONI**

**MADAI NAMBARI 408 YA 2020**

**Mimi VICTORIA FINANCE**
**Namdai**
**Mdaiwa DAVID KIMARO**

**Kwa: DAVID KIMARO WA MAKONGO JUU**

**Kwa kuwa mdaiwa/mdai/ameleta/wameleta/madai yake/yao kwamba**
**UNAAMRIWA NA MAHAKAMA HII KUHUDHURIA MAHAKAMANI BILA KUKOSA TAREHE ILIYOPANGWA**

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii ya SINZA tarehe 26/03/2021 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo, lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo. Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 25/02/2021.



**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

Ndugu **Florence M GOMBE** Anatangaza kupotelewa na Kadi ya gari aina ya **SUZUKI CARRY** Yenye namba za usajili **T426CWM. CHASSIS NO DC51T539456** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo Cha polisi. Taarifa ya polisi RB NO. **MOR/MOR/RB/87721/2021**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waziri Ndugulile sawa punguzo la tozo usajili mitandao isipokuwa...

**HIVI** karibuni, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, aliiagiza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kuangalia upya tozo za usajili wa mitandao ya kijamii.

Aidha, alitaka kuangalia uwezekano wa kupunguza gharama za usajili ili kutoa nafasi kwa vijana wengi kujiajiri, lakini kanuni ni kikwazo kikubwa kwa kuwa wengi hawana mtaji.

Alitoa siku 30 kwa TCRA kupitia sheria zote na kuhakikisha inaweka wazi muda wa usajili wa mitandao hiyo kuanzia sasa, ikiwamo kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mitandao.

Waziri huyo alitoa agizo hilo kwa kutumia mamlaka yake, hivyo hakuna anayeweza kudai kuwa alikuwa na maslahi binafsi badala ya ya Taifa. kisheria.

Agizo la waziri huyo linakuja siku chache baada ya TCRA kutangaza kusitisha usajili wa mitandao ya kijamii, ili kupitia upya waliosajili na kuona kama kuna umuhimu wa kusajili.

Suala la gharama za usajili ni kilio cha muda mrefu baada ya kukamilika kwa kanuni ya matumizi ya mtandao ambazo zimeelekeza malipo ya Sh. 100,000 hadi milioni moja kwa maudhui mtandaoni.

Kwa mujibu wa kanuni hizo kutangaza mtandaoni mubashara kwa radio na TV gharama zake katika ya Sh. 50,000 hadi 200,000, leseni zote zikitolewa kwa miaka mitatu.

Gharama hizo zimejikita kwenye maombi ya leseni, 'blog', 'Internet cafe', maudhui mtandaoni, foramu mbalimbali, radio na TV mtandaoni na mitandao ya kijamii.

Tangu kupitishwa kwa kanuni hizo kimekuwa ni kilio cha vijana wengi kushindwa kutimiza ndoto za kumiliki tovuti na mitandao kutoa maudhi kutokana na ada na tozo kubwa.

Vijana wengi hasa wa uandishi wa habari wameshindwa kujiajiri kutokana na kikwazo hicho, kwamba ndiyo amemaliza chuo anatakiwa kuwa na fedha za usajili, ada na vifaa vya kazi yake.

Wengi wana vifaa, lakini hawana ada na tozo, jambo linalozima ndoto zao kwa kuwa hata wakianzisha mtandao itachukua muda kupata matangazo ya kurudisha fedha kwenye uwekezaji wake.

Agizo la Waziri limekuja muda mwafaka kwa kuwa itatoa nafasi kwa wengi kujiajiri na kuchangia katika uchumi wa nchi, kuliko kuiingia katika matumizi mabaya ya mtandao.

Licha ya kupunguza gharama hizo kubwa, ni ufuatiliaji wa maudhui yanayorushwa mtandaoni ili yasiwe yenye kuharibu utamaduni, umoja na maadili ya Watanzania.


Kwa sasa kuna TV za mtandaoni ambazo nyingi maudhui yake siyo nzuri, na mbaya zaidi wengi wamejikita katika kupata watazamaji na wafuatiliaji kiasi cha kuwa na vichwa vya habari vya 'kupika' ili kumshawishi mtu kufungua naye kutengeneza fedha kupitia idadi ya watembeleaji.

Bila ufuatiliaji na nidhamu ya kinachosambazwa mtandaoni, kuna hatari ya kuiharibu au kuichanganya jamii, hasa vijana ambao wengi maisha yao ni kwenye matumizi ya teknolojia.

Tunatarajia serikali yetu sikivu italiona hilo na kulifanyia kazi, kwa kuwa imekuwa ikijipambanua kuhusiana na suala zima la kuongeza ajira kwa Watanzania, hususani vijana.

Kwa kufanya hivyo itakuwa imewasaidia na kuwawezesha kuongeza mipato chao sambamba na kujitengenezea ajira na watanzania wengine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Itapendeza tukiacha masikio yetu yajisafishe yenyewe

Na Sabato Kasika

**USAFI** na utunzaji wa masikio ni jambo muhimu katika afya ya binadamu na kutokana na ukweli huo, watu hutumia vitu mbalimbali, zikiwamo pamba, vijiti vya kibiriti, kalamu na vingine, lengo ni kufanyia usafi wa masikio yao.

Hata hivyo, inaelezwa kitaalamu kuwa masikio yana mfumo wake wa asili wa kujisafisha yenyewe. Hivyo, si sahihi kutumia kitu kingine kwa ajili ya kuyasafishia, badala yake yanatakiwa kuachwa yafanye kazi yake.

Inawezekana watu wakatumia vitu hivyo kufanya usafi wa masikio, kwa kuwa hawana taarifa sahihi kuhusu namna ya kutunza au kusafisha masikio, hayo ambayo wataalamu wa afya wanasema ni hatari.

Mtu anapochokonoa sikio lake, baadhi wakitumia kalamu, pamba, kijiti au kuweka mafuta ya wanyama, ni kinyume na utaratibu ambao mwili wa binadamu unao, ili kujisafisha kama ilivyo kiungo sikio.

Si vitu hivyo tu, bali wapo wengine wanatumia manyoya ya kuku kusafishia masikio yao. Kinachotakiwa ni kwamba, kuzingatiwe kanuni, mwongozo na taratibu za kiafya. Daima si sahihi kwa mtu kuingiza kitu chochote masikioni anapotaka kutoa uchafu.

Evelyna John, ni mwanafunzi wa mwaka wa tano wa fani ya udaktari katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), na panapo majaliwa baada ya kipindi cha mpito cha mazoezi kazini baada ya kuhitimu, atakuwa daktari kamili mwenye leseni yake.

Bado anahimiza kwamba, mtu hatakiwi kuingiza kituo chochote ndani ya masikio. Sababu kuu ni kwamba, vitu hivyo vinaweza kukatika au kusababisha kuchunika kwa mifereji ya masikio, kutoboa ngoma na kutengua mifupa iliyoko ndani ya masikio.

Msisitizo uliyopo kitaalamu ni kwamba, masikio yaachwe yajisafishe yenyewe, kwa kuwa kitendo cha kuyaingizia vitu, kinaweza pia kusababisha kupungua uwezo wa kusikia, kizunguzungu au dalili nyingine za maumivu ya masikio.

Anashauri watu waachie asili ifanye kazi yake, kwa kuwa uchafu ndani ya sikio hutoka wenyewe kulingana na asili ya ufanyaji kazi wa mwili, kwa vile miili yetu huzalisha nta masikioni ili yawe laini, safi na yenye ulinzi imara.

Inaelezwa kuwa uchafu, vumbi na vingine vinapoingia masikioni mwetu, hunasa au kukwama kwenye nta hiyo ambayo kazi yake ni kuhifadhi chembechembe zozote ili zisipenye ndani zaidi kwenye mifereji ya masikio.

Uchafu huo unapokwama, huwa unatoka wenyewe nje, hivyo ni muhimu kuyaachia masikio yafanye kazi yenyewe badala ya kutumia pamba, njiti za kibiriti na vitu vingine kusafishia.

Kwa kuwa miili yetu huzalisha nta masikioni ili kuyafanya kuwa laini, safi na yaliyo na ulinzi wa kutosha ili uchafu, vumbi na vitu vingine vinavyoweza kuingia ndani vinase kwenye nta hiyo, basi tuiachie nta ifanye kazi.

Aidha, inaelezwa kuwa matone ya maji yanaweza kuwa na faida ya kulainisha nta ndani ya masikio na kuondoa uchafu, lakini mtu akiwa na tatizo la kujaa nta, ni vyema akamuona daktari, badala ya kuchokonoa kwa pamba au kijiti.

Kulingana na maelezo hayo ya kitaalamu, ni wazi tunatakiwa kuachana na mtindo wa kusafisha masikio kwa mazoea, badala yake tuzingatie tunachoelezwa kwa ajili ya usalama wa afya ya masikio yetu.

Tunakumbushwa kuwa, si vibaya kutumia pamba kusafisha nje ya masikio, lakini siyo kuingiza ndani ambako kuna kawaida ya uchafu kutoka wenyewe kulingana na maumbile yetu. Sikio la nje linaweza kusafishwa kwa pamba au kitambaa kwa kufuta taratibu nyuma ya masikio na katika mafundo mbalimbali ya nje yake, bila ya kuingiza kidole au kitambaa kwenye mfereji wa masikio.

Masikio, yakiwa sehemu ya milango mitano ya fahamu, yana kazi ya kupokea mitetemo na mawimbi ambayo kwa pamoja huingia katika mchakato maalum unaoleta uwapo wa maana katika ubongo wetu.

Ni muhimu kuzingatia, tunaposafisha masikio, tuepuke madhara yanayotajwa. Wataalamu wameshatuwekea wazi kwamba, hakutakiwi pamba na vingine, kwani kuzipa nafasi tunakaribisha madhara.

## HABARI KITAIFA

# Vijana wahamasishwa usafi kwa kampeni

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPENI iliyopewa jina la 'Kijana Ni Usafi' ambayo inalenga kuhamasisha tabia ya usafi miongoni mwa vijana nchini, imezinduliwa mkoani Morogoro.

Kwa mujibu wa Augustino Dickso, mratibu wa mradi wa Raleigh Tanzania, kampeni hiyo ya miezi sita inayotekelezwa na Shirika la Msaada la Uingereza (UKAID) inalenga wanawake na wanaume wenye umri wa miaka 15-35.

Kampeni hiyo uliyozinduliwa jana, inatarajia kuwafikia vijana 48,000 katika mikoa minne ambayo ni Iringa, Dodoma, Dar es Salaam na Morogoro.

Alisema kampeni hiyo inakusudia kuhamasisha vijana kuzingatia tabia chanya za usafi kama kunawa mikono, kutumia maji salama, udhibitiwa taka na usafi binafsi, ili kufikia malengo ya kampeni ya Kijana Ni Usafi, Raleigh Tanzania ambao ndio waratibu. Kampeni hiyo imechagua na kuwajengea uwezo juu ya elimu ya usafi vijana 2,500 wenye ushawishi katika jamii.

Vijana hao kutoka katika mikoa minne iliyochaguliwa watatumika kuwajengea uwezo vijana wengine katika jamii zao ili kuhakikisha wanazingatia usafi, kwa mujibu wa Dickso, na kwamba kampeni hiyo imeundwa kwa kuzingatia mahitaji mahsusi ya usafi kwa kila mkoa.

Alisema kwa mfano mkoani Dar es Salaam, kampeni inalenga kuhamasisha udhibiti wa taka.

Mkoani Iringa kampeni imelenga pia kuhamasisha udhibiti wa taka, lakini kwa njia tofauti. Iringa wamechukulia taka kuwa fursa ya biashara.

Alisema mkoani Dodoma, imelenga kuhamasisha usafi binafsi kwa vijana, na kwamba kwa Morogoro, lengo kuu ni kuhimiza matumizi ya maji salama katika jamii.

Alisema sababu kubwa ni kwamba mkoa wa Morogoro umeathiriwa na magonjwa ya homa ya matumbo, kuhara na mlipuko wa kipindupindu mara kwa mara.

# Waziri aonya ununuzi holela viwanja

**Na Mwandishi Wetu,** MKURANGA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mwita Waitara, amewataka wananchi kujiridhisha kuhusu maeneo wanayotaka kununua kwa ajili ya makazi ili kuepusha migogoro inayoweza kujitokeza.

Waitara alitoa rai hiyo jana alipotembelea kiwanda cha nondo cha Fujian Hexingwa Co. Limited kilichoko Kisemvule wilayani Mkuranga mkoani Pwani.

Alisema kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa baadhi ya wananchi kuhusu uchafuzi wa mazingira hususani moshi unaotoka katika baadhi ya viwanda vinavyozunguka makazi ya watu kikiwamo kiwanda cha Fujian.

"Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya viwanda yawe ya viwanda. Sasa wananchi wakivamia maeneo haya, inakuwa kichaka cha malalamiko na kutaka kulipwa fidia.

"Idara za Mipangomiji zielimishe wananchi kuhusu maeneo hayo yametengwa kwa shughuli gani badala ya kuwaacha wajenge halafu waje kulalamika.

"Kama ikitokea mtu ameingilia kiwanda, akilalamika hatutamsikiliza. Mtu lazima ajiridhishe, je, ni halali? Kitu gani kimepangwa kujengwa katika eneo hilo?" Waitara alisisitiza.

Naibu waziri huyo pia aliwataka wamiliki wa viwanda kuajiri wataalamu wa mazingira ili kuwashauri wenye viwanda kuzingatia taratibu kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004.

Katika hatua nyingine, Waitara amemwagiza Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filberto Sanga, asimamie wananchi waliojenga kando ya kiwanda hicho watakapolipwa fidia ifikapo Machi 30, mwaka huu, wawe wameondoka katika eneo hilo ili waondokane na kelele zitokanazo na shughuli zinazofanyika kiwandani huko.

Vilevile, aliliagiza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), lifanye ukaguzi wa mara kwa mara katika kiwanda hicho ili kuhakikisha kinazingatia Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 ili kupunguza uchafuzi wa mazingira utakaoweza kujitokeza.

Mkuu wa Wilaya hiyo alisema malalamiko ya wananchi yanatokana na baadhi yao kununua viwanja kiholela ambavyo havijapimwa na Halmashauri ya Wilaya na viko karibu na maeneo ya viwanda.

Pia alitumia nafasi hiyo kuwaelekeza wataalamu wa ardhi na mipango miji kutoka wilaya hiyo, kuanza kutenga na kupima maeneo yatakayotumika kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda wilaya mwake.

Sanga alimshukuru Waitara kwa kufanya ziara kutembelea wilaya hiyo hususan katika kiwanda hicho ili kujionea vikwazo vya kimazingira kwa wananchi wanazonguka kiwanda hicho.

Kiwanda cha Fujian Hexingwa Co. Limited kinalalamikiwa na baadhi ya wananchi kuwa kinatoa moshi mzito pamoja kelele, hali inayoathiri mazingira na afya za wakazi wanaoishi karibu na kiwanda hicho.




Mshindi wa droo ya pili ya kampeni ya Bonge la Mpango ya Benki ya NMB, Yusuf Kyando, akipokea funguo za pikipiki ya matairi mitatu aina ya Lifan Cargo kutoka kwa Meneja wa NMB Kanda ya Kaskazini, Aikansia Muro (katikati), jijini Tanga jana. Kushoto ni Meneja wa Benki hiyo, tawi la Tanga, Elizabeth Chawinga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Akasirishwa kasi ujenzi chuo cha VETA

**Na Francis Godwin,** IRINGA

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, ametoa siku 20 kwa wasimamizi wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) Pawaga mkoani Iringa, kukamilisha kazi hiyo kabla ya kuchukua hatua kutokana na ucheleweshaji wakati serikali imeshatoa fedha.

Kipanga alitoa agizo hilo, juzi, baada ya kufanya ziara kukagua maendeleo ya ujenzi wa chuo hicho.

Alisema hajafurahishwa na kasi ya ujenzi huo hasa ikizingatiwa tayari serikali imeshatoa zaidi ya Sh. bilioni moja kwa ajili ya kazi hiyo.

Pamoja na kutoa siku 20, pia ametoa siku saba kwa Mkuu wa Wilaya ya Iringa kuiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufanya uchunguzi wa ujenzi wa chuo hicho hasa mafundi walivyopatikana na gharama iliyotumika kwa ujenzi kama ina uhalisia.

Alisema anashindwa kujua sababu ya kokoto za kujenga chuo hicho kutoka Dodoma wakati katika mkoa wa Iringa kuna kokoto za kutosha, hivyo lazima uchunguzi ufanyike na kupata majibu kwa nini zinunuliwe kwa gharama kubwa Dodoma na kuacha kokoto za Iringa.

"Wenzetu wa TAKUKURU watakuja na majibu sahihi kwa nini kokoto za kujenga Iringa zitoke Dodoma wakati Iringa kuna mawe ya kutosha kwa ajili ya kupata kokoto za kujengea chuo hicho," alisema.

Kipanga pia aliagiza VETA kumwondoa mhandisi kutoka makao makuu aliyekuwa akisimamia ujenzi huo na kumteua mtaalamu mwingine wa kufanya kazi hiyo.

Alisema ujenzi wa chuo hicho ni miongoni mwa miradi 25 ambayo inajengwa chini ya VETA katika wilaya 25 nchini lengo likiwa ni kuwezesha watoto watakaoshindwa kufaulu kwenda sekondari na wale wa kidato na nne watakaoshindwa kuendelea na kidato cha tano na sita kujiunga na vyuo hivyo kwa ajili ya kupata elimu ya ufundi.

"Ifahamike kuwa serikali kupitia bajeti yake ya mwaka 2019/20 ilitenga Sh. bilioni 40 kwa ajili ya kujenga vyuo hivyo katika wilaya 25 nchini ili kutoa fursa ya vijana wasiopata nafasi ya kujiunga na sekondari kupata ujuzi katika vyuo hivyo," alisema Kipanga.

Alisema kuwa mradi huo uko katika malengo ya serikali na ukiwa na bajeti yake pamoja na kuendelea kukarabati vyuo vya maendeleo ya jamii nchini kwa kutenga zaidi ya Sh. bilioni 7.9 kutumika katika uboreshaji wa vyuo hivyo nchini.

# Wananchi 23,000 kunufaika mradi wa majisafi na salama

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

ZAIDI ya wananchi 23,000 wa vijiji vitatu Sengerema mkoani Mwanza, wanatarajia kunufaika na mradi wa majisafi na salama.

Hayo yalibainishwa jana wilayani Sengerema na Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Cassian Wittike, wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Maji kimkoa iliyofanyika huko. Alitaja vijiji hivyo ni Kasenyi, Nyamahona na Mwaliga.

Alisema mradi huo ambao ulianza mwezi Mei, mwaka jana, unagharimu Sh. milioni 700 ambazo zilihusisha ujenzi wa vituo vipya 21 vya kuchotea, ununuzi wa mabomba, ukarabati wa vituo vinne, ufundi na vifaa.

Kuhusu mradi wa maji wa Tabaruka- Busulwangili, alisema utakamilika mwisho wa mwezi huu na zaidi ya wakazi wa 7,500 watanufaika.

Alisema mradi huo ulianza Aprili, mwaka jana, na unatarajia kukamilika mwishoni mwa mwezi huu na kwamba tangi hilo litakuwa na uwezo wa ujazo wa lita 90,000 za maji na umegharimu Sh. milioni 400.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Mwanza, Immaculata Raphael, alisema watatumia wiki ya maji katika kuweka mawe ya msingi katika miradi ya maji pamoja na kutoa elimu ya maji kwa watumiaji maji.

Raphael alisema mwaka jana walikamilisha miradi 10 katika wilaya ya Sengerema na kwamba watazindua miradi saba ya maji na kuwekewa mawe ya msingi kwenye miradi 17 katika wilaya hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Dk. Emmanuel Kipole, aliipongeza RUWASA kwa kukamilisha miradi ya maji katika wilaya yake.

Alisema kwa sasa maji yameanza kutoka katika vijiji vya Kalangaya na Butoto na kuwataka wananchi kutimiza wajibu wao katika kulipa ankara za maji.




Meneja Mwandamizi wa Huduma Mbadala wa Benki ya CRDB, Mangire Kibanda (katikati), akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa huduma ya kuhamisha fedha kwa wateja wanaobashiri kati ya akaunti ya benki hiyo na akaunti ya mtandao ya M-Bet (m-bet wallet), jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkurugenzi wa Masoko wa M-Bet, Allen Mushi (kulia) na Meneja wa Huduma ya SimBanking ya Benki hiyo, Emmanuel Moshi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# JKT kulima ekari 28,000 mazao chakula, biashara

**Na Renatha Msungu,** RUKWA

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) linatarajia kulima ekari 28,000 za mazao ya chakula na biashara kufikia mwaka 2024/25, ili kuliwezesha kujitegemea kwa chakula kwa asilimia 100 na kuuza mazao nje ya jeshi hilo.

Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Charles Mbuge, aliyasema hayo jana katika ziara yake kwenye Kikosi cha 847 Milundikwa JKT kilichoko wilayani Nkasi mkoani Rukwa.

Alisema mpaka sasa tayari vikosi hivyo vimelima ekari 12,247 na wanaendelea kuongeza ekari mwaka hadi mwaka mpaka kufikia malengo waliyokusudia.

Kutokana na juhudi zinazofanywa na jeshi hilo, alisema anaamini malengo hayo ya kulima ekari 28,000 ifikapo 2024/25 yatatimia, akibainisha kuwa Kikosi cha 847 Milundikwa kilitakiwa kulima ekari 1,300 za mahindi katika msimu huu, lakini kimevuka lengo kwa kulima ekari 1,500.

Kaimu Mkuu wa Utawala JKT na Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo Mkakati, Mifugo na Uvuvi, Kanali Hassan Mabena, alisema ili kufikia malengo hayo kwa asilimia 100, wamejiwekea mikakati ya kuboresha mashamba.

Alisema walianza na kilimo cha dharura mwaka 2019/20 na mwaka 2020/21 wameanza utekelezaji wa mpango mkakati wenyewe.

Alisema ili kutekeleza azma ya JKT, waliangalia vikwazo walivyopo kisha kuvitumia kama fursa kwa kununua zana bora za kilimo yakiwamo matrekta na zana zingine mbalimbali, ili kufanya kilimo chenye tija zaidi.

Mbali na hilo, alisema walikwenda katika taasisi za serikali zinazojishughulisha na masuala ya kilimo na kupata mbegu bora sambamba na kupima afya ya udongo katika mashamba yao yote.

Kamanda Kikosi cha 847 Milundikwa JKT, Luteni Kanali Philemon Mahenge, alisema licha ya kuvuka lengo katika msimu huu, bado wanatarajia kuongeza mashamba hadi kufikia ekari 2,000 ifikapo 2021/22.

Alisema lengo lao ni kuona wanafikia malengo waliojiwekea ya kujitegemea katika masuala ya chakula.

# Wanafunzi 6,000 wakatiwa bima afya

**Na Rose Jacob, MWANZA**

SHIRIKA la Plan International Tanzania limewakatia bima ya afya wanafunzi 6,000 wanaoishi katika mazingira magumu ambao wanasoma katika shule za msingi 37 za Nyamagana na Ilemela mkoani Mwanza.

Meneja wa Shirika hilo, Nelson Musikula, alisema jana kuwa watoto hao wamepatiwa kadi za bima ya afya kupitia mradi wa VUKA. Musikula alisema hayo katika kikao cha kamati ya huduma ya uchumi, elimu na afya ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

"Katika mradi wa VUKA tunafanya tathmini ya watoto wenye ulemavu wa kuona, kusikia na viungo, ambao hawana uwezo wa kwenda shule kutokana na kukosa vifaa muhimu vya kuwasaidia," alisema Musikula.

Aidha, Musikula alisema vifaa hivyo ambavyo vimekuwa vikichangia ukosefu wa elimu kwa watoto wenye ulemavu ni baiskeli, vifaa vya kusaidia kusikia pamoja na walimu wa kuwafundisha.

Musikula aliomba serikali kuwachukulia hatua wazazi wanaotupa watoto au kuwatelekeza mitaani, hali ambayo inazalisha watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya, Sikitu Sanziote, alishauri shirika hilo kushirikiana na madiwani wanawake ili kuwasaidia wanafunzi wa kike kwa kuwapatia mahitaji muhimu.

"Wanafunzi wa kike wakipata usaidizi wa kulinda afya zao huwa wanafanya vizuri darasani hivyo tunaomba shirika hili kutuunga mkono suala tulilolianzisha la kuwawezesha watoto wa kike kielimu ili kuwaepusha wasipate mimba," alisema Sanziote.

Naye Diwani wa Nyegezi, Edithi Mdogo, aliomba shirika hilo kuwasaidia watoto waishio kwenye mazingira magumu hususani katika stendi za mabasi na vituo vya daladala.

HABARI KITAIFA

## Kampuni kuikusanyia Songea ushuru mazao

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

Halmashauri ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma imeingia mkataba na kampuni ya West Food Comp LTD ya Makambako mkoani Njombe kukusanya ushuru wa mazao.

Makubaliano ya mkataba huo yalisainiwa na Mkurugenzi wa Kampuni na uongozi wa Halmashauri.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Tanu Kameka, aliitaka kampuni hiyo kufanya kazi waliyoomba kwa ufanisi kwa sababu Serikali inategemea mapato kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake.

Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Godwin Chengula, aliahidi kufanyakazi kwa ufanisi, na kwamba ana uzoefu katika kazi ya ukusanyaji ushuru ambayo ameifanya katika maeneo ya wilaya za Ulanga, Ifakara , Makambako na Manispaa ya Songea

Naye Mweka Hazina wa Halmashauri, Rajabu Lingoni, alisema katika kuboresha ukusanyaji wa mapato, vikao vya kisheria vilikubaliana kumpata mzabuni atakayefanya kazi ya ukusanyaji wa ushuru wa mazao, badala ya kuendelea kuwatumia mawakala.

"Maamuzi hayo yamefikia baada ya kubaini udanganyifu mkubwa katika ukusanyaji wa ushuru,unaofanywa na baadhi watendaji wa kata kupitia mawakala wao, kitendo ambacho kilikuwa kinakwamisha jitihada za Halmashauri katika kutekeleza majukumu yake," alisisitiza.

## Mikopo yadhibiti ukatili wa kijinsia

**Na Shaban Njia,** SHINYANGA

ASILIMIA 10 ya fedha za mikopo inayotolewa na Halmashauri ya Shinyanga Vijijini kwa vikundi vya wanawake, vijana na walemavu, imesaidia kupunguza ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto chini ya miaka 18.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, halmashauri hiyo ilitenga kiasi cha Sh. milioni 150 na kutoa Sh. milioni 144.6 kwa vikundi vya wanawake wajasiriamali, vijana na watu wenye ulemavu katika kata 26, vijiji 126 na vitongoji 856.

Katika mgawanyo wa mikopo hiyo, vikundi vya wanawake 13 vilipata Sh. milioni 70.6, vijana vikundi vitano Sh. milioni 52.6 na vikundi vitano vya watu wenye ulemavu viliipata Sh. milioni 21.3 huku mwaka huu wa fedha zikiwa zimetengwa Sh. milioni 200 na kati ya fedha hizo hadi sasa zimeshatolewa Sh. milioni 64 kwa vikundi 11.Hayo yalibainishwa na Kaimu Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Didia, Maliam Chungwa, alipozungumza na vyombo vya habari vinavyotekeleza mradi wa nafasi ya vyombo vya habari katika kumaliza ukatili dhidi ya wanawake na watoto unaotekelezwa na SPC kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania (WFT).

# Mfumo kuvutia vijana kwenye kilimo waanza

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, amezindua mfumo wa Kizimba 'Business Model' ukiwa ni mkakati wa kuwavutia vijana katika kilimo na kuendeleza kilimo biashara kwa kuongeza tija kwenye mnyonyoro wa thamani wa mazao ya kilimo.

Mfumo huo unaratibiwa na Ushirika wa Wajasiriamali Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUGECO) ikiwa ni sehemu ya mkakati wa chuo kuhakikisha wahitimu wake wanajiendeleza kwa vitendo kupitia ushirika huo ili kuleta mageuzi makubwa katika sekta ya kilimo.

"Naomba nitoe wito kwa taasisi za kifedha kutoa mikopo yenye masharti nafuu ili kufanikisha utekelezaji wa mfumo huu wa kizimba kwa kuwavutia vijana wengi," alisema.

Prof. Mkenda ameupongeza mfumo huo na kusema utasaidia kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao ambayo ni chachu katika uanzishaji na uendelezaji wa viwanda.

Amesema kwa sasa kilimo kinachangia theluthi moja kwenye pato la taifa tofauti na idadi ya zaidi ya theluthi mbili ya ushiriki wa Watanzania katika sekta ya kilimo, hali inayopelekea kuwapo kwa ugumu katika kumkwamua mkulima kutoka kwenye umaskini.

Alikipongeza Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kwa kuwa mama wa SOGECO na mchango wake ni mkubwa katika sekta ya kilimo.

Mkurugenzi Mtendaji wa SUGECO, Revocatus Kimario, alisema mfumo huo umelenga kutengeneza mnyororo wa thamani wa zao husika kulingana na uhitaji wa soko, hivyo kuwaweka wakulima pamoja ili kupata mahitaji yatakayowezesha kupata mahitaji yatakayowezesha tija ya uzalishaji kupatikana.

"Malengo yetu ni kusogeza huduma muhimu za mkulima katika eneo moja ili kufanya urahisi wa upatikanaji wa mahitaji tofauti na kumuhudumia mkulima mmoja mmoja na hii ni kwa sababu ya changamoto za miundombinu," alisema Kimario.

Mmoja wa wahitimu katika chuo hicho ambaye ni mnufaika wa SUGECO, Yohana Tewa, alisema mpango huu utakwenda kutatua changamoto za masoko ya mazao yanayozalishwa nchini na kukifanya kilimo kuwa miongoni mwa sekta zitakazosaidia kuondoa tatizo la ajira.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa madarasa mapya katika Shule ya Msingi Busekera, Wilaya ya Musoma, mkoani Mara juzi, ambayo kwa sasa ina madarasa 10, wakati mahitaji halisi ni 24. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Onyo wanaowageuza mtaji wenye ulemavu

**Na Yasmine Protace**

MWENYEKITI wa kikundi cha watu wenye ulemavu (MWAKAYE) kilichoko Kivule, Dar es Salaam, Rehema Said, ameiomba serikali iwachukulie hatua watu wanaowabeba watoto wenye ulemavu katika baiskeli wakiwa na makopo kuwageuza kuwa ombaomba.

Mbali na kuwageuza watoto hao kuwa ombaomba, pia fedha ambazo zinapatikana watu hao huzitumia kwa manufaa yao.

Rehema aliyasema hayo katika ufungaji wa mafunzo ya siku tano ya uraghibishi yaliyotolewa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

"Naiomba serikali, iwachukulie hatua hao watu wanaobeba watoto walemavu na kuwadhururisha maeneo mbalimbali kuomba fedha na zinapopatikana wanazichukua," alisema.

Aliongeza kuwa utafiti alioufanya na ikaonekana watu wanawachukua watoto wenye ulemavu vijijini na kuja nao mjini kuwadhururisha kuomba fedha na zikipatikana wanachukua wao.

Alisema watoto wanayo haki ya kupata elimu, lakini kuwadhururisha na kuchukua fedha haki ya mtoto inakuwa imepotea.

Alisema mtoto mwenye ulemavu anahitaji haki kama mtoto mwingine, anatakiwa kwenda shule ikiwamo kupata mahitaji ya msingi badala ya kumficha ndani.

"Katika kufanya utafiti nikagundua mtoto anatolewa kijijini kuletwa Dar es Salaam na kutembezwa ili wazazi wanufaike na fedha," alisema.

Akizungumzia mafunzo ya uraghibishi, alisema kuwa ameweza kujifunza jinsi ukatili wa kijinsia unavyofanywa ndani ya familia.

# Lishe duni yatajwa chanzo watoto wenye vichwa vikubwa

**Na Beatrice Moses**

LISHE duni kwa wajawazito na watoto wachanga, imetajwa kuchangia kuwapo kwa ongezeko la watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi, hali ambayo inaibebesha mzigo wa gharama za matibabu serikali.

Ofisa Jamii, Teresia Jacob, alisema Tanzania bara ndiyo inaongoza kwa kuzaa watoto wenye matatizo hayo katika mikoa ya Morogoro, Dodoma, Pwani na Iringa.

Alisema takwimu za mwaka 2018, Taasisi ya Tiba ya Mifupa, Mgongo, Ubongo na Mishipa ya Fahamu (MOI) kwa wiki wanapokea watoto wenye matatizo hayo kuanzia watano hadi sita.

Jacob alisema idadi hiyo inaweza kuwa ni kubwa, lakini inaweza kupunguzwa ama kufutwa kwa ushirikiano wa wazazi na jamii kwa ujumla kuzingatia lishe bora kwa wajawazito na watoto wachanga.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, aliziagiza halmashauri zote kuhakikisha kwenye bajeti ya mwaka 2019/2020 kila halmashauri kutenga shilingi 6,000,000 ili kushughulikia matibabu watoto wenye kichwa kikubwa na mgongo wazi.

Alisema hayo Oktoba 2018, Jafo alipowahutubia wananchi kwenye maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Watoto wenye Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi Duniani iliyofanyika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

Alisema fedha hiyo itasaidia kuwapatia matibabu kwa wakati hudumia watoto 30, hatua ambayo itasaidia kupunguza matatizo yanayowakabili watoto hao nchini.

Meneja mradi wa Taasisi ya Kimataifa ya Global Alliance for Improve Nutrition(GAIN), Archard Ngemela, alipokuwa akizungumza wakati wa mafunzo kwa wanahabari kutambua umuhimu wa kushiriki katika kuielimisha jamii kuzuia vyanzo vya matatizo hayo kwa watoto, alisema

mojawapo ni pamoja na kuhimiza viwanda vya unga wa ngano na mahindi kurutubishwa nafaka hizo ili kuwa bora kwa watumiaji hasa wenye manufaa kwa wajawazito na watoto.

"Ni muhimu kutumia chumvi iliyowekwa madini joto kwenye chumvi na mafuta yaliyowekwa vitamini A, bidhaa zilizoongezwa vitamini husika huwa na nembo maalum na inajulikana," alisema.

Katibu Afya Mkoa wa Dar es Salaam, Sister Mathew, akizungumza kwa niaba ya Mganga Mkuu wa Mkoa huo, aliwasihi waandishi wa habari kushikiri kikamilifu katika kuielimisha jamii ikiwamo kuwahamasisha wajawazito kuhudhuria kliniki mapema ili wapate ushauri pamoja na dawa zenye folic acid zinazosaidia kuimarisha lishe.



Wakazi wa Goba Tegeta A kwa Madawa, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam, wakichota maji yasiyo safi na salama jana, kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kutokana na eneo hilo, kukosa huduma ya maji salama ya bomba. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Bil. 14/- zaongeza kipato kwa kaya maskini Singida

**Na Elisante John,** SINGIDA

SERIKALI imetumia zaidi ya Sh. bilioni 14 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Singida kati ya Septemba 2014 hadi sasa, kwa ajili ya miradi ya maendeleo na kuongezea kipato kwa jamii ya wilaya hiyo kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini uliopo chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Hayo yamebainishwa na ofisa mwezeshaji na ufuatiliaji wa TASAF wa Wilaya ya Singida, Simith Haule, wakati wa kujionea mafanikio na changamoto mbalimbali kutoka kwa wanufaika wa mpango huo, katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida.

Alisema licha ya malipo kwa kaya maskini zaidi, kiasi kingine kilitumika kutekeleza miradi ya maendeleo, ukiwamo ujenzi wa mabwawa na barabara kwa walengwa kulipwa fedha baada ya kufanya kazi za ajira ya muda.

Baadhi ya wanufaika akiwamo, mkazi wa Kijiji cha Ilongero msichana Amina Nyambi (26), alisema amefanikiwa kuongeza thamani ya mtaji wa ufugaji hadi kufikisha kuku zaidi ya 40 kutoka vifaranga nane alioanza nao Mei mwaka jana.

Msichana huyo alibainisha kuwa licha ya kuku hao, amefanikiwa kuongeza mtaji hadi kufikisha Sh. 400,000 kutoka Sh. 240,000 alizoanza nazo, hivyo kuongeza wigo wa biashara zake.

Alifafanua licha ya kuwa na ndoto ya kupanua zaidi banda lake ili aweze kuongeza shamba la kuku, ametoa wito kwa wasichana wengine kuhakikisha wanatumia fursa zilizopo kwa kujiajiri katika biashara ili kukabiliana na changamoto za maisha.

Mratibu wa TASAF Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Piyazs Tindikali, alisema mpango wa kunusuru kaya maskini nchini unahudumia walengwa 7,178 katika halmashauri hiyo.

# Wajasiriamali kicheko TBS kufungua ofisi kwenye kanda

**Na Mwandishi Wetu**

WAJASIRIAMALI wamepongeza uamuzi wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kufungua ofisi za kanda kwamba zimewarahisishia kupata huduma ikiwamo uthibitishaji ubora.

Awali, wafanyabiashara hao walilazimika kusafiri hadi Dar es Salaam, yaliko makao makuu ya shirika hilo kwa ajili ya kupata huduma hiyo.

Wajasiriamali hao walitoa kauli hiyo jana kwa nyakati tofauti wakati wakizungumza kwenye maonyesho ya Bidhaa za Viwanda vya Wanawake Tanzania yaliyoandaliwa na Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC).

Maonesho hayo yaliyoanza Februari 26, yalimalizika jana kwenye Viwanja vya Posta, Kijitonyama, Dar es Salaam.

Akizungumza kwenye maonyesho hayo, mmiliki wa Kampuni ya RUMZAHRAIM Investment ya Mtwara, Rukia Liumba, alisema TBS kufungua ofisini kwenye kanda kumewafanya wawe karibu na shirika hilo."Sasa hivi hatuogopi tena TBS, popote tunapokuwa wanakuwapo hata kwenye maonyesho kama haya, lakini hata ule usumbufu wa kutoka mikoani kuwafuata makao makuu haupotena," alisema Liumba.Alitoa mfano kuwa siku za karibuni alikumbana na changamoto kwenye uzalishaji wa bidhaa zake, lakini kwa sababu TBS wako,Mtwara, ilikuwa rahisi kwake ku-wafuata na kumsaidia tatizo lake.

Kuhusu faida alizopata tangu alipopatiwa leseni ya kutumia alama ya ubora wa TBS, Agosti, mwaka jana, alisema bidhaa yake ya unga wa mhogo imezidi kupata soko tofauti na awali.

# Tathmini kaya 220 kulipwa fidia mgodini

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

JUMLA ya kaya 220 zinazoishi ndani ya mgodi wa dhahabu wa Buckreef Gold Company LMD mkoani Gaita zinafanyiwa tathmini ili ziweze kulipwa fidia kupishaji uzalishaji wa mgodi huo ndani ya miezi 6.

Akizungumza na wananchi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye eneo la mgodi huo, jana, Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni ya Buckreef Gold Campany LTD, Isaac Bisansaba, alisema wanategemea kufanya tathmini eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 9.4 ambalo lina jumla ya kaya 220 na zoezi hilo linategemea kuchukua wiki sita mpaka nane.

Bisansaba alisema: "Zoezi hili ni sehemu ya matakwa ya sheria inatutaka kama mgodi kuhakikisha kwamba majirani zetu wote wanaozunguka mgodi huu wanafanyiwa thathmini ya haki na kiwango kinachotakiwa na kwa muda mwafaka."

Aidha, alisema tathmini hiyo itahusisha vijiji vitatu Mneke, Rwamgasa na Kibada ambavyo vipo kwenye kata za Rwamgasa, Busanda na Kaseme na zoezi hilo linaanza baada ya Mkuu wa Wilaya ya Geita kuamua lianze jana.

ama

ALHAMISI MACHI 18, 2021

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

## WIKI YA MACHO

## Mabingwa Muhimbili, CCBRT wamchambua mpofushaji namba mbili, presha ya macho



Ukurasa 14

## KWANINI MAMA ANAKATISHA KUNYONYESHA?

## Wenyewe wasimulia ya moyoni, huku daktari bingwa akifunguka

# Siku tano za Naibu Waziri wa Maji Mbeya zenye neema kwa wakazi

### •Atumia mguu kilomita kukagua •Pia wapo hawakuachwa salama

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MWANZONI mwa mwaka huu, Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, alifanya ziara kukagua miradi ya maji katika halmashauri sita za mkoa wa Mbeya.

Hapo aliambatana na maofisa wa wizara hiyo, watendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya- WSSA), watendaji wa Wakala wa Usambazaji wa Maji Vijijini (RUWASA), kuanzia ngazi ya taifa mpaka wilaya na viongozi wa kisiasa.

Naibu Waziri huyo pamoja na maofisa walioambatana, walipanda milima na kushuka mabonde kuvifikia vyanzo vya maji vinavyopeleka huduma kwa wananchi, ambako ujenzi unaendelea, lengo ni kujiridhisha na uwapo wake.

Yapo maeneo walitumia miguu umbali zaidi ya kilomita moja, ndipo walifikia vyanzo, kutokana na kuwa palikuwa pagumu kufikia kwa usafiri wa gari.

Huko kuliibuka shangwe za wananchi, kutokana na kuwapa matumaini ya kuanza kunufaika na miradi ya maji na katika maeneo mengine, iliwatikisa mameneja wa RUWASA kutokana na kushindwa kusimamia miradi ma hata baadaye, baadhi waliondolewa katika nafasi zao.



Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi (kushoto), akikagua mradi wa kisima wa Ilongo Group wakati wa ziara mkoani Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

**DC MBEYA**

Siku ya kwanza ya ziara ya Naibu Waziri Mahundi, ilianzia Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, alikotembelea kata mbili, alikofahamishiwa kuwa vijiji sita katika Kata ya Iwindi na viwili kata ya Igale, havipati huduma ya maji, liche ya kuwapo miradi mitatu, ambazo serikali zilishatoa zaidi ya Sh. bilioni 3.5 za kuikamilisha.

Hapo ndipo Mahundi alipotoa siku 14 kwa Meneja wa RUWASA wilayani Mbeya, Mhandisi Hans Patrick, azikamilishe katika vijiji sita vya kata ya Iwindi na mwezi mmoja kwa meneja wa mamlaka hiyo, kukamilisha katika vijiji vya kata ya Igale.

Pia, aliahidi kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa agizo hilo, ili kuhakikisha maeneo hayo yanaondokana na tatizo la wakazi kufuata maji katika umbali mrefu.

"Katika vijiji vya Igale na Shongo, serikali imetoa Sh. milioni 20 kwa ajili ya kununua mashine ya kusukuma maji kwa sababu kule ni milimani. Lengo la serikali ni kumtua mwanamke ndoo ya maji kichwani, kwa hiyo harakisheni," anasema Mahundi.

Ni safari iliyoendelea katika kata ya Swaya, ambako kwa muda mrefu kuna kilio cha wananchi wa baadhi ya vijiji kukosa huduma ya maji, wengine wanapata mgawo kwa sababu ya kutokamilika mradi.

Katika kata hiyo, kuna mradi uliofanyiwa usanifu miaka 10 iliyopita na ulitarajiwa kufuta tatizo la maji, lakini mpaka sasa haujatekelezwa, wakazi wake wakilalamika zaidi.

**Inaendelea Uk. 12**

AFYA

# Siku tano za Naibu Waziri wa Maji Mbeya zenye neema kwa wakazi

Inatoka Uk. 11

Naibu Waziri anasema, mradi unapaswa kufanyiwa usanifu upya, kwa sababu ya ongezeko la watu tofauti na ilivyokuwa awali, ili unapotekelezwa ukidhi mahitaji stahii.

Katika hilo, anamwagiza Meneja wa RUWASA abuni chanzo kipya, endapo usanifu unaotolewa utaonyesha kuwa maji hayo hayatoshelezi.

**ZIARANI CHUNYA**

Siku ya pili, ziara ya Naibu Waziri umbali wa kilomita 300 kutoka Mbeya Mjini, katika Kata ya Matwiga Chunya, alikozuru Bwawa la Matwiga linalokusudiwa kuvikomboa vijiji 16. Hata hivyo, umekwama kwa miaka 16 sasa.

Huko, alikagua bwawa lililokamilika muda mrefu, mabomba yamehifadhiwa, uchimbaji mitaro, uunganishaji mabomba na akashiriki ujenzi wa tangi la kuhifadhi maji, kabla ya kuwasambazia watumiaji.

Anawaambia wanavijiji kwamba, wataanza kunufaika na mradi ambao serikali ilishatoa Sh. bilioni 2.5 wakitakiwa kuukamilisha hadi ifikapo mwisho wa mwezi huu.

Huku akitambulisha kuufahamu vizuri mradi huo na matatizo yake, kwamba hata kabla ya kwenda kugombea ubunge na kuteuliwa kuwa Naibu Waziri, alikuwa Mkuu wa Wilaya hiyo kwa mwaka mmoja na nusu.

Mahundi aliweka jiwe la msingi kwenye Mradi wa Maji wa Makongorosi, kunakotarajiwa kumaliza tatizo la maji lililoko huko, eneo lenye utajiri wa madini ya dhahabu.

Anaagiza mkandarasi mjenzi alipwe fedha zake, ili aongezewe kasi, kwani ametumia fedha zake kujenga tangi lililofika zaidi ya asilimia 80.

Katika hilo, Meneja wa RUWASA wilayani Chunya, Mhandisi Ismail Nassor, anawahakikisha kuufuatilia kwa karibu miradi tajwa, ili ukamilike haraka na kuwanufaisha wananchi mara moja.

**WILAYANI RUNGWE**

Naibu Waziri Mahundi, wilayani Rungwe alikagua miradi mitatu, wa Masoko Group unaokusudiwa kuhudumia vijiji 13, akikiri kuvutiwa nao na akaiagiza RUWASA iiboreshe, ili uvihudumie vijiji vingi zaidi.

Pia, alizuru mradi wa Lukata uliodumu kuchukua miaka mitano ikigharimu zaidi ya Sh. milioni 30, walengwa ni vijiji viwili, aambako alitamka kukerwa zaidi kwa kukosa ufanisi, huku akiwashangaa wataalamu wanaoutelekeza, wakiomba fedha zaidi za usanifu wa mradi mwingine.



Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi (kushoto) na Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Usambazaji Maji Vijijini (RUWASA), Mhandisi Clement Kivegalo, wakishiriki kuchanganya zege kwa ajili ya ujenzi wa tangi la kuhifadhi maji kwenye Mradi wa Bwawa la Maji la Matwiga, wilayani Chunya. **PICHA ZOTE: NEBART MSOKWA.**

Ni ziara aliyosonga nayo katika mradi ndani ya Halmashauri ya Busokelo, akiwa na ufafanuzi: "Tunataka wananchi wapate maji, sasa naagiza RM (Meneja wa RUWASA Mkoa) kuunda timu ya wataalamu waje wafanye uchunguzi hapa, ili mradi utekelezwe haraka na wananchi waanze kupata maji."

Katika Mradi wa Kandete, iliyoko Mwakaleli, Busokelo, alikuta ujenzi wa chanzo umekamilika, lakini shida ni usambazaji maji kwa wananchi, ndiko nako akaagiza Meneja wa RUWASA wilayani Rungwe aukamilishe ndani ya mwezi mmoja, wananchi wapate huduma.

**ACHACHAMAA KYELA**

Ni kati ya wilaya zenye vyanzo vichache vya maji, hivyo miradi mingi inavitegemea vyanzo vilivyopo katika Halmashauri ya Busokelo.

Naibu Waziri wa Maji Mahundi, alizuru chanzo cha maji kilichofanyiwa utafiti na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), pakabainika kuwa na uwezo wa kumaliza tatizo la maji katika miji ya Kyela na mpakani Kasumulu.

Kiongozi huyo anawapa matumaini wananchi wa miji hiyo na vijiji vinavyopitiwa na mradi huo, kuwa serikali itahakikisha inakamilika na kuanzaa kupata huduma mapema.

"Wataalamu wamesema zinahitajika Sh. bilioni 3.5. Sasa mimi naahidi kuwa, serikali itatoa fedha hizo kwa awamu, ili mradi ukamilike na mimi nitafuatilia bila ya hata kutoa taarifa, ili nione utekelezaji," anasema Mahundi.

Mkurugenzi wa Mbeya-WSSA, Mhandisi Ndele Mengo, anawahakikishia kuwa fedha zikitolewa watauukamilisha ndani ya miezi 18.

Mhandisi Mengo, ambaye sasa ni Mkurugenzi wa RUWASA taifa, anasema utafiti walioufanya ulibaini mahitaji ya maji katika miji hiyo ni lita milioni nane kwa siku, lakini mradi huo una uwezo wa kuzalisha lita milioni 15, hivyo kuna ziada ya lita milioni saba .

Naibu Waziri aliwaagiza watendaji wa RUWASA wa Kyela, kufufua miradi iliyokuwa ya DANIDA, ambayo miundombinu yake imechakaa, ili zisaidie kukabiliana na uhaba wa maji katika baadhi ya maeneo.

**MBARALI PAMOTO**

Akiwa wilayani Mbarali, hakuficha kuona kukerwa zaidi namna miradi ya maji wilayani humo haiendelei, huku akilalamika watendaji wa RUWASA wakitoa taarifa amazozitaja zisizo sahihi.

Malalamikio ya Naibu Waziri ni namna miradi mitano ilivyotafuna fedha nyingi za serikali, huku wananchi bado hawanufaiki nayo na katika Mradi wa Ruduga-Mawindi uliopo kijijini Kanganga, alibaini mabomba kutelekezwa tangu Oktoba mwaka jana.



Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi (kushoto), akikagua uunganishaji wa mabomba ya kupeleka maji kwa wananchi katika mradi wa maji wa Bwawa la Matwiga wilayani Chunyawa kunufaisha vijiji 16.

Pia alimlalamikia aliyekuwa Meneja wa RUWASA wakati huo, kutochukua hatua za uendelezaji tangu mwezi Agosti Mwaka jana hadi mwanzo wa mwaka huu.

Z|iara hiyo, iliendana na ukagua mradi wa maji unaohudumia mji wa Rujewa, akija na hoja kwamba haukutoa maji kwa zaidi ya miezi miwili, wananchi wakinywa maji yatokanayo na 'skimu' za umwagiliaji.

Ni hatua iliyoendana uamuzi mgumu wa kuivunja Bodi ya Maji ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Rujewa na kumwagiza Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA, Mhandisi Clement Kivegaro, kumwondoa Meneja wa Wilaya hiyo kwa kushindwa kusimamia miradi.

"Kila mradi tunaotembelea huku ni kichefuchefu, sasa naivunja Bodi ya Maji Rujewa na naagiza iundwe mpya ambayo haitakuwa na mjumbe hata mmoja aliyekuwmo kwenye hiyo ya awali. Huyu Meneja wa RUWASA pia hatufai," alitamka Mahundi.

**UMAUZI MGUMU**

Ni ziara iliyoendana nma tamko la uamuzi mgumu, baada ya Naibu Waziri kutamka alibaini miradi mingi ya maji kitaifa inalega haikamiliki kwa sababu ya uzembe wa meneja wa RUWASA wa wilaya zao.

Anasema, hatua inayofuata ni kwa wizara itaanzisha mpango wa kuwaondoa meneja wasiojiweza nchi nzima na kuajiri wapya wenye uwezo, akitamka wengi waliopo ni waliokuwa wahandisi wa maji kwenye halmashauri kabla ya RUWASA kuanzishwa, eanafaya kazi kwa mazoea.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri huyo, hadi sasa kuna vijana wengi walip chini ya meneja hao na wana uwezo mkubwa wa kusimamia miradi, hivyo serikali itaangalia uwezekano wa kuwapandisha ili wawahudumie wananchi kwa ufanisi.

Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, Suma Fyandomo na Mkurugenzi wa RUWASA (wakati huo), waliahidi kufuatilia kwa karibu miradi yote ambayo naibu waziri alitembelea, kuangalia utekelezaji wa maagizo aliyotoa hayo.

Ni ziara ambayo baada a muda iliendana na mameneja wawili mkoa wa Mbeya kuondolewa, huu baada ya muda mfupi Mkurugenzi wa RUWASA, Mbeya kupandishwa cheo katika nafasi kitaifa.

AFYA

WIKI YA MACHO

# Mabingwa Muhimbili, CCBRT wamchambua mpofushaji namba mbili, presha ya macho

## •Wengi wanatembea na shida hawajijui

**Yasmine Protace na Maulid Mbaga**

MIONGONI mwa vitu vinavyotajwa kusababisha matatizo ya macho ni vumbi, moshi, kupigwa na kitu machoni, upasuaji ambapo wataalamu wamebainisha kuwa njia hiyo ya matibabu nayo inaweza kusababisha tatizo lingine.

Aidha, kitaalamu vinatajwa vyanzo vya kukaa sehemu zenye mwanga mkali, zikiwamo zenye mionzi ya jua na inayotokana na kemikali zenye asili ya kutoa mwanga kwa njia ya mlipuko wakati wa kuchomwa, sambamba na matumizi ya kompyuta kwa muda mrefu.

Wataalamu wanasema huwagusa pia watu wenye kawaida ya kufikicha au kugusa macho na vidole vyao wakati wa kutoa uchafu, hali inayotajwa nayo sio salama kiafya, ikihimizwa mbadala wa kitambaa chepesi au maji masafi.

Kuna tahadhari inayotolewa na wataalamu wa afya ya jicho, kwamba kuna haja ya kuwa makini katika kulinda kiungo hicho, hasa kwa wanaotekeleza majukumu yao ya kila siku.

Anataja mazingira hatarishi kama viwandani, migodini na watumiaji kompyuta, huku wanaopenda kukaa karibu na televisheni, au wanaopigwa na miale ya jua kwa muda mrefu.

Hapo ndipo kuna ushauri wa kijihami kitaalamu, kwamba walioko viwandani wanashauriwa kuwa na utaratibu wa kuvaa miwani, pale penye mwanga mkali na walioko migodini, wanapaswa kuepuka kugusa macho na mikono yenye vumbi.

Ni mtazamo unaofikia kwa waliko ofisini wasipende kutumia kutumia kompyuta zikiwa na mwanga mkali na inapotokea tofauti machoni, wanapaswa kumuona daktari haraka.

Katika mujumuisho ulioko, wataalamu wanaeleza kuwa ugonjwa mmojawapo unaochangia upofu watu wengi bila ya kujijua ni presha ya macho, ambayo dalili zake huja kwa kujificha.




Mkuu wa Idara ya Macho wa Hospitali ya CCBRT, Dk. Cyprian Ntomoka, akitoa elimu ya ugonjwa wa presha ya macho, kwa wananchi hospitalini hapo. **PICHA: YASMINE PROTACE**

**KUTOKA CCBRT**

Ugonjwa wa presha ya macho una madhara makubwa, iwapo matibabu yake yatachelewa kutolewa kwa mgonjwa kwa wakati, athari yake mojawapo ni kutoona vizuri au kupofuka.

Katika maadhimishoya Siku ya Presha ya Macho katika Hospitali ya CCBRT, Dar es Salaam kwa kushirikiana na Asasi ya DunPharma, yaliyochukua siku tatu kati ya Machi 10 hadi 12, katika viwanja vya hospitali hiyo, mengi yalijitokeza, yakiendana na upimaji bure.

Dk. Cycpian Ntomoka, Mkuu wa Idara ya Macho wa CCBRT, anasema wagonjwa wengi wanaoletwa hospitalini matatizo yao ya presha yanakuwa yamechelewa kuanza matibabu, kwa kiwango anachokitaja asilimia 70 hadi 80, mishipa ya fahamu ya macho inakuwa imekufa.

Anasema mishipa inapokufa, wataalamu hawawezi tena kuirejeshea uwezo na wanabaki kupigania kilichosalia ndicho ili wakinusuru nacho kisipoteze uoni wake.

"Glaucoma ni ugonjwa ambao unaumiza mishipa ya fahamu ya macho, ambayo unachukua taarifa za jicho kwenda kwenye ubongo. Ni ugonjwa unaosababisha upungufu wa kuona au ulemavu wa kuona kama hautatibiwa kwa wakati," anasema.

Anasema, tafiti zote zilizofanywa duniani, zinaonyesha sehemu kubwa ya wagonjwa wanakutwa na presha ya macho iliyozidi.

**INAKUWAJE KUUGUA?**

Dk. Ntomoka, anasema presha ya kawaida ya macho kitaalamu inapaswa kuwa katika kiwango anachokitaja kati ya 10 na 21, wengine mishipa imekufa kubakia asilimia tano ya uwezo.

Anasema, tabia ya jicho inaanza kupoteza uoni wa pembeni na inapofika katikati linakufa kabisa, hivyo ana ushauri katika kupambana na maradhi hayo, jamii inatakiwa kujenga utaratibu wa kujikagua ubora wa macho yao.

Mtaalamu huyo anashauri kila mwenye miaka 40 na zaidi, anatakiwa walau mara moja kila baada ya miaka miwili na wenye miaka 65 na zaidi ni kila baada ya miezi sita.

Pia ndani ya familia iwapo upo mwenye tatizo, kuna uwezekano wa karibu mwingine kuugua, hivyo uchunguzi wa kila mara ni muhimu.

Kwanini mtoto anpatwa na shida ya macho? Dk. Ntomoka anasema wao tatizo linaanza katika mfumo wa kuumbwa kwake tumboni kwa mama.

Kwa mujibu wa daktari huyo bingwa, presha ya macho ni ya pili duniani kwa kusababisha upofu usiotibika na hutokea mshipa wa fahamu unaopeleka mawasiliano kwenye ubongo, unaposhambuliwa kutokana na presha kali na matibabu ya awali, ndio yanawezesha ama tatizo kumalizika au kupungua.

Dk. Ntomoka anazitaja dalili za presha ya macho ni pamoja na kuona rangi za upinde wa mvua unapoangalia taa; kupungua uwezo wa kuona pembeni; kupoteza uwezo wa kuona kabisa, macho na kichwa kuuma, macho kuwa makubwa au kioo cha jicho kuwa cheupe (kwa watoto).

"Hapa kwetu CCBRT tunayo kliniki maalumu ya presha ya macho mara tatu kwa wiki na katika kila kliniki, tunapokea wagonjwa wa presha ya macho kati ya 40 na 45.

"Wengine hujitokeza siku zisizo za kliniki wakihitaji kuonana na daktari wa macho kwa shida hiyo, hii inatoa taswira ya ukubwa wa tatizo," anasema.

Anataja mbinu ya kwanza, ni kujenga tabia ya kufanya uchunguzi wa afya ya macho mara kila mara na kama mtu katika jamii yake kuna historia ya ugonjwa huo, hivyo kunapaswa familia kufanya uchunguzi wa macho mapema.

Inapoonekana mtoto anafikicha sana macho yake, yanayotoa machozi na kuonekana makubwa, anapaswa kupelekwa kwenye kituo cha afya au hospitali ya karibu kwa ajili ya uchunguzi, ikiendana na matumizi mazuri ya dawa za macho kadri utakavyoshauriwa na daktari.

Kuhusu matibabu, bingwa huyo wa macho CCBRT anasema inatibiwa kwa vidonge, dawa ya matone, upasuaji, matibabu kwa njia ya kipandikizi na mionzi.

**BINGWA WA MUHIMBILI**

Daktari bingwa wa Upasuaji wa

Endelea Uk. 14



Mgonjwa akihudumiwa hospitalini. **PICHA: MTANDAO.**

AFYA

## KWANINI MAMA ANAKATISHA KUNYONYESHA?

# Wenyewe wasimulia ya moyoni, huku daktari bingwa afunguka ukweli ulivyo

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

ELIMU ya unyonyeshaji inahitajika ili kuwaondolea kinamama dhana ya maziwa kuharibika na kukatisha huduma hiyo, kwa watoto walio na umri chini ya miaka miwili.

Mara nyingi kuna hali zinazokinzana kutoka kwa wanyonyeshaji upande mmoja na wataalamu wa afya upande wa pili. Je, ukweli uko wapi kati ya madai hayo yanayosigishana?



Mama mkazi wa Mwanza akiwahudumia watoto wake. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

**KUTOKA KWA DAKTARI**

Dk. Maduhu Nindwa, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Magu, anaiambia Nipashe kwamba tatizo la kuharibika maziwa halipo na ndio maana mtu anapopata ujauzito anashauriwa aendelee kunyonyesha mpaka atakapokaribia kujifungua.

Tabibu huyo anahimiza kwamba, kuharibika maziwa ni dhana isiyo na ukweli, hasa kwa mtoto hasa wenye mwaka na miezi kadhaa, kunaweza kuchangiwa na sababu mbalimbali, ikiwamo kupungua umakini wa usafi, namna anavyolishwa chakula na vyombo vya kumlishia.

Pia anataja upungufu katika umakini, kwa sababu kipindi hicho ndicho mtoto anaanza tabia ya kula udongo unaoweza kumsababishia kula wadudu kama minyoo, amiba hata akaishia kuharisha.

Dk. Nindwa anawataka wanawake kuzingatia maelekezo wanayopatiwa kliniki ya mtoto, kwani wanapaswa kumpeleka huko hadi atakapofikisha umri miezi 59 sawa na miaka mitano, kasoro mwezi mmoja.

Anasema, katika kipindi hicho kunafanywa mwendelezo kwa kumpima uzito, lishe, chanjo za aina mbalimbali pamoja na kupatiwa ushauri wa vyakula sahihi vya kutumia, kwa ajili ya ukuaji wa ubongo.

"Tunawashauri waendelee kunyonyesha kwa miaka miwili, wasiache, kwani kuna faida nyingi ikiwamo mtoto kunyonya kwa muda mrefu anatengeneza urafiki na mama yake.

"Pia kutobeba mimba kama hajafuata uzazi wa mpango. Kwa kunyonyesha tu, baadhi inawasaidia sana, lakini siyo wote, kwani kunyonyesha kwa nguvu, mwili hauwezi kuzalisha mayai ya kuweza kubeba mimba. Tunasisitiza walau anyonye miaka miwili mfululizo," anasema Dk. Nindwa.

Mtaaluma huyo anafafanua kwamba kuna haja ya mtoto akinyonya maziwa ya mama pekee kuanzia siku ya kwanza hadi miezi sita na baada ya hapo, kuanzia mwezi wa saba aendelee kunyonya akichanganyiwa na chakula mbalimbali, ili kuujengea mwili kinga ya kukabiliana na magonjwa.

**SIMULIZI YA MZAZI**

Wonde Richard (28) ni mkazi wa Butuja, wilayani Ilemela, jijini Mwanza. Ni mama wa watoto wanne waliopishana mwaka mmoja na nusu, huku akiwa na mimba inayokaribia kujifungua.

Anasimulia anavyositisha huduma ya kunyonyesha kwa dhana ya 'maziwa kuharibika' huku kuna umbali wa kituo cha afya kuchangia kutompeleka mtoto kliniki, kabla ya kutimiza umri miaka miwili.

Wonde anasema, huwa ana kawaida ya watoto wanapofikisha mwaka mmoja na miezi mitatu na nusu, anaanza kuhara kila mara kila anapomnyonyesha.

Mama huyo anasema, kuna elimu aliyopatiwa na wazazi wake kwamba, hali kama hiyo inapojitokeza ni dalili ya maziwa kuharibika, hivyo achukue uamuzi wa kusitisha huduma hiyo.

Anaeleza uamuzi mkuu anaochukua ni kuchemsha mchicha pasipo mafuta na 'makorombwezo' mbalimbali kwa ajili ya mlo wa mchana akiwa na watoto wake, huku jioni akitarajia kula viazi vitamu vilivyochemshwa.

Mama Wonde anasema, pia huwa anaangukia kikwazo hicho huku kuna shida ya umbali wa kituo cha afya kinachangia kutompeleka mtoto kilinki na imechangia watoto wake wote akawasitisha na huduma ya kliniki, kabla ya kufikisha umri miaka miwili.

"Huyu mdogo ana mwaka mmoja tu. Ukweli nimechoka kumpeleka kliniki! Umbali unachangia tunatembea kwa miguu ukizingatia nina ujauzito mwingine, lakini nikipata nafasi naenda naye," anasimulia ulivyo mkasa wake.

"Huku kwetu 'zoezi' la kumpeleka kliniki mtoto limekuwa la mazoea ya mtu kupenda, japokuwa serikali inasisitiza miaka mitano" anasema, akiwa na ufafanuzi wa hatua inayofuata ni kumwachisha mtoto uji." anaongeza.

Katika hatua inayofuata, anasema mbadala wake hapo ni kuanza kumpa mtoto chakula cha viazi, huku akikiri wanawake wengi wanazingatia utolewaji sindano zenye umuhimu kwao ikiwamo ya mwezi mmoja hadi mitatu, miezi tisa na mwaka na nusu.

**WATOTO WANALELEWAJE?**

Anasema lishe ya kila siku ya watoto wake kwa kuwapatia uji usio na sukari muda wa saa sita; saa tisa mchana ugali na mchicha; ilhali na mlo wa usiku ambao haufafani.

Hata hivyo, mama huyo ana angalizo kwamba, mara kadhaa huwa wanakula mara moja, pindi hali ya uchumi inakuwa ngumu.

"Kubwa ni hawa watoto waliofuatana kupigana mara kwa mara, kwa sababu hawapatani. Hivyo, wakianza kupigana tunawaacha tu kufuatilia ugomvi wao unachosha, wakiumizana ndio tunawauliza mbona mnapigana," anaeleza.

Mama huyo ana ombi kwa kiserikali kwamba, iongeze na kuboresha huduma za wajawazito na watoto, ili ziwe ubora zaidi na dawa zipatikane.

Pia ana malalamiko ya mfano imekuwa kawaida wanapofika katika maeneo ya matibabu kwa watoto wanapofikishwa wagonjwa, wanaishia kupewa dawa za maumivu kama Panado wakitakiwa wajitegemee kununua dawa zingine wanazoelekezwa na daktari.

Wonde anasema kuna wakati wanakosa fedha na mtoto anabaki anaumwa pasipo kupata msaada, pia anashauri watoa huduma wawe wachangamfu, kuacha hulka za ukali zinazowakatisha tamaa na kuwaondolea, wazazi na wagonjwa kwenda kliniki, akiwa na msisitizo maalum ya kujengwa urafiki na wajawazito.

Lucas Bulenganija ni Balozi katika Mtaa wa Butuja, anasema kwamba elimu ya afya ya uzazi ni muhimu, ili kunusuru malezi duni ya watoto, hasa kwa watu wa maeneo ya mialo (pwani ziwani).

"Japokuwa elimu inatolewa lakini nguvu zaidi inahitajika ili watu watumie uzazi wa mpango kuondoa wimbi la watoto na mama waweze kuwapa huduma zote, ikiwamo kunyonyesha mfululizo.

"Uzazi wa mpango unasaidia kutobebanisha watoto. Tatizo ni wengine wakishagundua ni wajawazito, wanawaachisha watoto hata akiwa na umri mdogo," anaeleza Bulenganija.

Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Severine Lalika, ana rai kwa jamii iendelee kupokea elimu na kuondokana na mtazamo uliokuwapo, ili kujenga taifa lenye afya na makuzi bora kwa watoto.

Anasema, katika maeneo ya mihalo kunakabiliwa na magonjwa mbalimbali, yakiwamo kuhara pamoja na matumizi mabaya ya kemikali, kwenye shughuli za uvuvi.

Mkuu wa Wilaya anasema kuna kawaida mustakabali yanayogeuka kuwa na madhara kwa binadamu, hivyo wataalamu huwa wanaenda katika maeneo hayo kutoa elimu ya namna ya kuthibitisha na kupambana na magonjwa yanayojitokeza, sambamba na kuwapa elimu ya afya ya uzazi wananchi.

# Mabingwa Muhimbili, CCBRT wamchambua mpofushaji namba mbili, presha ya macho

**Inatoka Uk. 13**

Macho kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, Neema Daniel, anasema presha ya macho, kuna wakati mtoto anaweza akazaliwa na tatizo hilo, pale sehemu yake ya kutoa machozi haitakuwa vizuri, pia anasisitiza jamii kuweka jitihada za kuufahamu ugonjwa huo kwa kwenda vituo vya afya kwa ajili ya kupima.

"Presha ya macho inasababisha mkandamizo kwenye mshipa wa kuona na hilo ndilo linalosababisha mtu kushindwa kuona na wakati mwingine humfanya mtu kupata upofu wa kudumu," anasema.

Pia anafafanua kitaalamu kuwa, kuna maji yanayotumika kusafisha jicho, ambayo pia yanafanya kazi ya kulisha zile sehemu ambazo mishipa ya damu haipiti kwa sababu mbalimbali.

Dk. Neema anasema, baada ya kusafisha maji hayo yanatakiwa kutoka na yasipotoka, ndioa tatizo linapoanza, huku akiwa na ufafanuzi kwamba, linaweza kumpata mtu yeyote, katika rika za utoto, kijana na mtu mzima.

Anataja mzizi wa tatizo ni pale kuna mambo yanapingwa machoni na mtu akiwa na umri mkubwa zaidi, kufahamu kama an tatizo hilo au hana, ni lazima akapime.

Daktari Neema anahitimisha kwa wito, kwamba Watanzania kuwa makini katika kukilinda kiungo hicho, na muhimu kutumia miundominu waliowekewa na serikali, kupaa huduma za tiba kitaifa.

**WALIOCHUNGUZWA**

Jamila Juma, mkazi wa Msasani, Dar es Salaam, alichukua hatua kwenda kutibiwa, baada ya kupata taarifa kupitia vyombo vya habari kuwapo huduma ya bure, CCBRT.

"Tumekuja na familia yangu wote hatuna tatizo. Tumepewa ushauri juuya kupambana na ugonjwa huona sasa tumeelewa ni muda gani inatakiwa ufanye vipimo,| anasema.

Hamis Maulidi, mkazi wa Magomeni Mapipa, Dar es Salaam, anahimiza tiba ya macho kutopuuzwa, badala yake uwe utamaduni wa kupima macho kila mara.



# Taasisi yalaani uzushi mitandaoni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TAASISI inayojishughulisha na masuala ya amani Tanzania (TPF), imelaani tabia ya baadhi ya watu kutumia vibaya mitandao ya kijamii kuzusha mambo ambayo yamekuwa yakiwachafua viongozi wakuu wa nchi hali ambayo inahatarisha amani.

Mwenyekiti Taifa wa Taasisi hiyo, Sadick Godigodi, aliyasema hayo wakati akizungumza kwenye kikao na semina elekezi kwa viongozi wa ngazi ya taifa pamoja na kanda kilichofanyika jijini Dodoma.

Alisema wao kama taasisi inayojihusisha na masuala ya kulinda amani, wanalaani vitendo hivyo, ambavyo vimeoneka kushamili hivi sasa katika mitandao ya kijamii.

Godigodi alisema kutumia mitandao ya kijamii kuchafua viongozi wakuu wa nchi na mambo mbalimbali yanayoihusu Tanzania haipaswi kufumbiwa macho. "Niwaombe Watanzania kuendelea kuipigania nchi yetu na kuacha kuwapa nafasi watu ambao wanaonekana kuwa hawana mapenzi na nchi yetu," alisema Godigodi.

Vilevile, alisema kuwa Watanzania wanatakiwa kuyapuuza mambo yote ambayo yamekuwa yakizushwa kwenye mitandao na kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kufikia malengo waliyojiwekea.

"Hizi ni kelele za barabarani hatuwezi kupunguzwa kasi na kelele hizi inabidi tuwapuuze kwani tukiwasikiliza tutapunguza mwendo sisi tunatakiwa kuwaunga mkono viongozi wetu wakuu wa nchi yetu katika mipango ambayo taifa limepanga kufikia kimaendeleo," alisema mwenyekiti huyo.

Akizungumzi kuhusu amani, alisema kila Mtanzania anao wajibu wa kuilinda na siyo kuiachia serikali.

"Kila mtu anao wajibu kulinda amani yetu katika kanisa, msikiti na eneo lolote lile kila mmoja wetu atimize wajibu kwani amani siyo jambo la mtu mmoja wala serikali pekee yake," alisema.

Naibu Katibu Mkuu Taifa wa TPF, Muslim Mputa, alisema kila mtu anatakiwa kutambua kuwa analojukumu la kulinda amani iliyopo ili isipotee.

Aidha, alisema taasisi hiyo tangu ianzishwe imepata mafanikio kadhaa ikiwamo kusaidia kutatua migogoro katika maeneo mbalimbali nchini.

"Kama ambavyo mtakumbuka ule mgogoro wa nani anaruhusiwa kuchinja sisi tulisaidia katika kutafuta suluhu lakini katika suala la mahakama ya kadhi jambo lile lilikwenda vizuri na mpaka hivi sasa Watanzania sisi ni wamoja," alisema Mputa.

Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Zainabu Issa, alitoa wito kwa taasisi hiyo kuendelea kutoa elimu juu ya kulinda amani pamoja na kukemea vitendo vya ukatili wa kijinsia.

"Ninaomba pia mjitahidi kutoa elimu juu ya vitendo vya ukatili wa kijinsi hivi sasa watoto wananyanyaswa, wanawake lakini wanaume wanapigwa sana bila kuripoti sehemu yoyote ile," alisema Issa.



Mchumi wa Jiji la Dodoma, Rozalia Hhari, akichangia mada kwenye warsha ya mfumo wa sheria ya elimu jumuishi kwa viongozi wa serikali za mitaa, iliyoandaliwa na mradi wa Free Pentecostal Church Tanzania, jijini humo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Siku 5 kuondoa mifugo eneo la mnada

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, ametoa siku tano kwa wafanyabiashara wa mifugo ambao wamekuwa wakihifadhi mifugo yao inayokwenda machinjioni katika eneo la mnada Kizota jijini Dodoma, kuiondoa kwa kuwa wanakiuka taratibu zilizowekwa.

Gekul alitoa agizo hilo alipotembelea mnada huo kwa lengo la kukagua shughuli zinazofanyika na kukutana na baadhi ya wafanyabiashara wa mifugo.

Gekul alisema zipo taratibu za uendeshaji wa minada ya upili ambapo mifugo ikishanunuliwa inatakiwa kuchukuliwa badala ya kutuzwa kwenye eneo hilo ikisubiri kupelekwa machinjioni.

"Natoa siku tano kwa wafanyabiashara wote ambao mnatunza mifugo yenu hapa mkisubiri kuipeleka machinjioni kuhakikisha mnaitoa na kuitafutia eneo jingine kwa ajili ya kuitunza," alisema.

Hata hivyo, alisema Wizara imeshatenga zaidi ya Sh. milioni 200 kwa ajili ya kuanza kuboresha miundombinu ya mnada huo ukiwamo ujenzi wa ukuta unaozunguka mnada huo.

Alitoa rai kwa wananchi kutovamia eneo la mnada, kwa kuwa ni moja ya sababu iliyochelewesha kuanza kwa ujenzi wa ukuta huo kutokana na kuwapo kwa migogoro iliyotokana na uvamizi wa ardhi.

Aliwataka viongozi katika ngazi ya kata, mitaa na vijiji kuhakikisha wanasimamia na kuchukua hatua mapema pale wanapoona mtu anavamia maeneo hayo ya minada.

Naye Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alisema timu ya wataalamu inayofanya uhakiki wa eneo lililovamiwa itakapomaliza kazi yake, watahakikisha wanalipima eneo hilo haraka.

# Waikataa kampuni ya upimaji wa ardhi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKAZI wa Mtaa wa Ndachi, Kata ya Mnadani jijini Dodoma, wameikataa kampuni ya upimaji wa ardhi ya Goe Salfes kwa madai ya kutowashirikisha wananchi katika upimaji viwanja kwenye eneo hilo.

Aidha, wakazi hao wamekubaliana kuandika muhtasari wa yale waliyokubaliana katika mkutano wa hadhara na kupeleka Rais John Magufuli ili awasaidie.

Hatua hiyo imefikiwa na wakazi hao kutokana na Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, kutoa udhuru kupitia kwa Ofisa Mipango Miji, Mohammed Said, ambaye alimwakilisha katika kikao kilichoandaliwa na wananchi hao hivi karibuni.

Katika kikao hicho, Saidi aliyemwakilisha Mkurugenzi alidai kuwa Mkurugenzi hawezi kufika katika eneo hilo kutokana na kuumwa, hali iliyosababisha wakazi hao kucharuka kwa madai kuwa wamekuwa na malalamiko ya muda mrefu kuonewa na kampuni hiyo, na walitaka wayawasilishe kwa mkurugenzi mwenyewe na si mwakilishi.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi hao, Mwenyekiti wa Mtaa wa Ndachi, Joyce Abel, alisema wamechoka kila siku kupigwa kalenda na mkurugenzi, hivyo wameamua kuandika muhtasari wa yale ambayo wamekubaliana na watampelekea Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Rais Magufuli.

"Maamuzi yetu ni kuwa mimi nimeajiriwa na wananchi, nipo kwa ajili ya wananchi, hatuitaki kampuni ya upimaji ilipewa muda lakini ni miaka mitatu haijafanya kitu chochote sisi tutampelekea muhtasari wa hichi kikao Waziri na Rais, maana Mkurugenzi wa Jiji ameshindwa kutusikiliza," alisema.

Vilevile, alisema kampuni ya upimaji iliyopewa tenda na Jiji la Dodoma haiwashirikishi wananchi, hivyo kwa kauli moja wamekubaliana kuikataa.

Alisema kwa sasa watu wanakaa katika nyumba zilizobomoka kutoka na Jiji kutokutoa vibali vya ujenzi hali ambayo imekuwa ikiwapa wakati mgumu.

Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Mnadani, Paul Bankiye, alisema wamekuwa wakiishi kama watumwa katika nchi yao kutokana na kutokupewa vibali vya ujenzi huku wananchi wakizungushwa kupimiwa viwanja vyao.

"Tunaenda kwa Rais tumechoka ardhi ndio mwokozi wetu, hatuitaki kampuni ya upimaji inazingua sana ina muda mrefu hakuna kitu chochote ilichofanya," alisema.





## Kanisa lawasilisha msaada hospitalini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KANISA la Victorious lililoko katika Kata ya Iduda jijini Mbeya, limetoa msaada wa mashuka 60 katika Hospitali ya Jiji hilo ya Igawilo ili kukabiliana na upungufu wa vifaa hivyo hospitalini huko. Waumini wa kanisa hilo walikabidhi msaada huo kwa uongozi wa hospitali hiyo juzi na kuomba mashuka hayo yatumike kwa ajili ya kuwasaidia wagonjwa wanaokwenda kutibiwa hospitalini.

Mchungaji wa Kanisa hilo, Adolphina Kapanga, alisema mashuka hayo yalinunuliwa kutokana na michango ya waumini wa kanisa hilo walioko katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mbeya pamoja na watu wengine wasiokuwa waumini wa kanisa hilo.

Alisema kanisa hilo limekuwa likiwashirikisha waumini wa makanisa mengine na wasioabudu, kuchangia michango mbalimbali ya kuwasaidia wahitaji mbalimbali wakiwamo wagonjwa na kwamba wao hawabagui mtu yeyote.

"Tumetoa mchango huu kwa lengo la kuwasaidia wenzetu wanaougua na kulazwa hapa, tumechangishana sisi wenyewe pamoja na kuwaomba wenzetu wa nje ya kanisa letu na wakaitikia tukapata haya mashuka 60 ambayo leo tumekuja kukabidhi," alisema.

Mchungaji Adolphina alisema mbali na mchango huo kwa hospitali hiyo, pia mwaka huu wamewasaidia watoto 20 wenye mahitaji maalum wakiwamo yatima, michango mbalimbali ya kuwawezesha kwenda shuleni.

Alisema utaratibu huo umekuwa unafanywa na kanisa hilo kwa mwaka wa pili huku baadhi ya waumini wake wakisema kutoa misaada kwa wasiojiweza ni sehemu ya matakwa ya dini na kwamba wataendelea kutoa misaada hiyo kila mwaka kulingana na mahitaji ya maeneo mbalimbali.

Mmoja wa waumini hao, Irine Erasto, alisema kanisa hilo linatamani kuendelea kusaidia zaidi lakini kinachokwamisha ni uchumi mdogo na kwamba wataendelea kutoa kila wanapopata.

"Ukisoma Biblia, inasema dini iliyo safi, isiyo na taka ni kuwasaidia yatima na wajane katika shida na dhiki zao. Kwa hiyo na sisi tuliliangalia kwa jicho la pili tukaona tusaidie kwa kidogo tulichopata," alisema Irene.

Diwani wa Iduda, Pishon Talaban, alisema msaada huo umesaidia kupunguzia Halmashauri ya Jiji la Mbeya gharama za kununua mashuka huku akiyaomba makanisa mengine kujitolea.

Akipokea msaada huo, Kaimu Mganga Mkuu wa Hospitali ya Jiji Igawilo, Dk. Richard Uria, aliushukuru uongozi wa kanisa hilo kwa kuamua kuelekeza msaada huo katika hospitali hiyo kwa kuwa utasaidia kuongeza ubora wa huduma. Alisema watahakikisha mashuka hayo yanatumika kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa wanaotibiwa hospitalini hapo. Aliwaomba wadau wengine wenye uwezo, kujitokeza na kusaidia shughuli mbalimbali katika hospitali hiyo ili kuboresha huduma zinazotolewa kwa wananchi.



Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Charles Mbuge, akiangalia miche ya zao la kahawa katika moja ya kitalu kilichoko ndani ya Kikosi cha 844 JKT Itende, jijini Mbeya juzi. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Bunge latoa miezi mitatu taasisi kulipa pango ardhi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, imetoa miezi mitatu kwa taasisi za serikali na binafsi zinazodaiwa kodi ya pango la ardhi na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kulipa madeni hayo.

Vilevile, kamati hiyo imeiagiza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuandaa orodha ya taasisi hizo zinazodaiwa madeni hayo na kuikabidhi kwa kamati hiyo ili iwe rahisi kufuatilia mchakato wa ulipaji wa madeni hayo.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Aloyce Kwezi, alitoa agizo hilo juzi wakati kamati ilipohitimisha ziara yake mkoani Mbeya, akibainisha kuwa katika ziara hiyo, walibaini kwenye mkoa huo pekee, taasisi hizo zinadaiwa zaidi ya Sh. bilioni 5.1.

"Tumeona tu hapa Mbeya ambapo ni mfano, TAZARA pekee wanadaiwa zaidi ya Sh. bilioni 1.9, Tanganyika Parkers wanadaiwa Sh. bilioni 1.4. "Sasa tunafikiria kwamba kama Mbeya peke yake taasisi hizi zinadaiwa fedha hizi, Tanzania nzima kwenye mikoa taasisi hizi zinadaiwa fedha nyingi sana," Kwezi alisema.

Baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo walisema taasisi zinazodaiwa fedha hizo, zinatakiwa kupelekwa kwenye Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ili zikaguliwe na kulazimishwa kulipa madeni hayo haraka.

Mmoja wa wajumbe hao, Hawa Mwaifunga, alisema baadhi ya taasisi hizo zimekuwa zikipata hati safi, lakini zinadaiwa madeni makubwa na wizara.

Alisema madeni hayo wangekuwa wanadaiwa wananchi wa kawaida, kuna uwezekano wangekuwa wametaifishiwa mali zao, lakini kwa sababu ni taasisi za umma, hatua hiyo haichukuliwi, hivyo akaitaka wizara kuongeza nguvu ya kuzidai.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, alikiri uwapo wa taasisi nyingi za umma nchini zinazodaiwa madeni makubwa na wizara hiyo na akaahidi kuwasilisha orodha ya taasisi hizo kwa kamati.

Alisema baadhi ya taasisi hizo zimepangishwa ardhi na serikali na zenyewe zikapangisha kwa watu wengine ambao zinakusanya kodi bila kuwasilisha serikalini na hivyo kuendelea kujilimbikizia madeni kwa muda mrefu.

Dk. Mabula alisema uamuzi wa kamati hiyo kuingilia kati kudai madeni hayo, utaisaidia wizara kukusanya madeni hayo kwa wakati na kuzielekeza fedha kwenye shughuli zingine za maendeleo.

"Ukiangalia hizi taasisi zina wapangaji ambao ukiwafuata kila mwaka wanalipa lakini zenyewe hazileti serikalini.

"Kama wizara, tutashukuru sana kama mtatusaidia kudai na niwaahidi ndugu wajumbe kwamba nitawaletea orodha hasa ya wadaiwa wakubwa," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema wizara inatakiwa kuushirikisha uongozi wa mkoa kwenye kudai madeni hayo ili kuongeza nguvu kwa kuwa zipo wizara zilizofanya hivyo na zikafanikiwa.

Alisema taasisi za serikali katika mkoa huo zilikuwa zinadaiwa zaidi ya Sh. bilioni 1.6 za ankra za maji na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA) lakini mamlaka hiyo ilipoishirikisha ofisi yake, taasisi hizo zimelipa zaidi ya Sh. bilioni 1.5 na zinaendelea kulipa.

# Waliokatiwa maji wapewa masharti

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI waliokatiwa huduma ya maji jijini Mbeya kutokana na madeni ya muda mrefu ya ankra, wametakiwa kutia saini mikataba maalum iliyoandaliwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA) ili warejeshewe huduma hiyo na kuanza kulipa madeni yao kidogo kidogo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mbeya-WSSA, Gilbert Kayange, aliyasema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Maji jijini Mbeya iliyofanyika katika chanzo cha maji cha Mto Nzovwe ambako shughuli mbalimbali za utunzaji wa vyanzo vya maji, ukiwamo upandaji miti, zilifanyika.

Alisema wananchi waliositishiwa huduma hiyo watatakiwa kulipa nusu ya deni na kwamba deni linalobakia, watatakiwa kulipa kidogo kidogo wakati wakiendelea kupata huduma hiyo ya maji.

Kayange alisema ili kuwasaidia zaidi wananchi, mamlaka hiyo imeamua kuondoa gharama za urejeshaji wa huduma hiyo ambazo zilikuwa zinatozwa awali.

"Ofa hii ni ya siku saba pekee ambazo ni za ndani ya maadhimisho ya Wiki ya Maji, na tunawataka wananchi kuchangamka ili warejeshewe huduma hii muhimu kwa maendeleo yao," alisema. Baadhi ya wananchi waliohudhuria uzinduzi huo na kushiriki kwenye upandaji miti katika chanzo hicho, waliiomba mamlaka hiyo kuweka utaratibu mzuri wa malipo kwa maelezo kuwa wakati mwingine wanabambikiwa madeni tofauti na matumizi halisi ya huduma hiyo.

Mmoja wa wananchi hao, Jackson Mwangobhe, alisema kitendo hicho ndicho kinachowafanya baadhi ya watu kutolipa madeni yao kwa wakati na kusababisha kusitishiwa huduma hiyo muhimu.

"Wangekuwa wanatoza tozo za kawaida, kusingekuwa na tatizo, lakini sasa unakuta mtu unatozwa gharama kubwa ambazo huwezi kumudu, ukishindwa kulipa mwezi mmoja madeni yanaanza kupandana na kufikia hatua ya kukatiwa huduma," alisema Mwangobhe.

Filbert Mndendemi aliuomba uongozi wa Mbeya-WSSA kuweka utaratibu wa kuwataarifu wananchi kabla ya kusitisha huduma kwa kuwa kusitisha huduma hiyo bila kutoa taarifa, kunawaumiza wananchi.

Vilevile, aliiomba mamlaka hiyo kuwapa taarifa wananchi kuhusu marekebisho yoyote kwenye vyanzo vya maji ili wajiandae kwa kujaza maji ya kutumia kwenye vyombo kuepuka madhara ya kukosa huduma.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mbeya-WSSA, Edna Mwaigomole, aliwataka wananchi wanaoishi jirani na vyanzo vya maji, kuvilinda vyanzo hivyo ili vitumike kwa muda mrefu.

Aliwataka kusaidiana na mamlaka hiyo kuilinda miti inayopandwa ili istawi na kusaidia kuvilinda vyanzo hivyo viendelee kutoa huduma hiyo muhimu.



# Utata kigogo anayetuhumiwa rushwa kuendelea na kazi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MVUTANO wa viongozi waandamizi Wizara ya Kazi, Uchumi na Uwekezaji umeibuka baada ya Ofisa Mwandamizi wa Kamisheni ya Kazi, Khamis Omar, kuendelea na kazi licha ya kukabiliwa na kesi ya tuhuma ya kupokea rushwa ya shilingi milioni moja, mwaka 2020.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake Mwanakwerekwe, Kaimu Kamishna wa Kazi, Suleiman Khamis Ali, alisema kesi hiyo imewahi kutokea, lakini msemaji wa suala hilo ni Mkurugenzi wa Uendeshaji na Utumizi wa Wizara, Januari Fussi.

"Jambo hili msemaji wake Mkurugenzi wa uendeshaji na utumishi kwa sababu yeye ndio mratibu wa mambo ya watumishi, mimi sina taarifa za suala hilo," alisema Suleiman.

Hata hivyo, Mkurugenzi wa Uendeshaji na Utumishi wa Wizara, Januari Fussi, alisema msemaji wa suala hilo ni Katibu Mkuu wa Wizara, Mussa Haji.

Alisema Kamisheni ya Kazi na Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) ni mamlaka zinazojitegemea licha ya kuwa zipo chini ya wizara, lakini Katibu Mkuu ndio msemaji wa mambo ya wizara yakiwamo ya watumishi.

"Katibu Mkuu ndio bosi wangu na jambo hili nimewahi kusikia kupitia mitandao ya jamii na vyombo vya habari, lakini mpaka sasa sijawahi kupokea barua ya kutaarifiwa kutoka Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar," alisema Fussi.

Alipotakiwa kuzungumzia suala hilo, Katibu Mkuu Mussa Haji, aliwataka waandishi wa habari kumuona Kaimu Kamishna wa Kazi kutokana na mtumishi huyo kuwa chini ya idara yake.

"Kwa jambo hilo mwoneni Kamishna wa Kazi, lakini kesi hiyo naikumbuka imewahi kutokea mwaka 2020," alisema Katibu Mussa, ambaye kabla ya uteuzi mwaka huu alikuwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA).

Kwa upande wake, Ofisa Uhusiano wa ZAECA, Yussuf Juma, alisema kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi, kiongozi au mfanyakazi anapotuhumiwa kwa kesi ya jinai kama ya rushwa na ufisadi anapaswa kusimamishwa kazi.

Akizungumza na wafanyakazi wa ZAECA hivi karibuni, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussen Ali Mwinyi, alisema serikali ya awamu ya nane itahakikisha kiongozi au mtendaji anayetuhumiwa kwa rushwa au ufisadi anasimamishwa kazi ili kupisha uchunguzi kufanyika.

Ofisa Mwandamizi wa Kamisheni ya Kazi, Khamis Omar, alikamatwa na ZAECA, akipokea rushwa ya shilingi milioni moja kama sharti la kutoa kibali cha kazi kwa raia wa kigeni mwaka 2020.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Ikulu jana, wakati wa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa maagizo yake, aliyoyatoa kwa mawaziri na makatibu wakuu. **PICHA: IKULU**

# Mwili wa mvuvi aliyezama waopolewa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KIKOSI Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM) na Kikosi cha Zimamoto na Uokozi vimeopoa mwili wa marehemu Hamdu Khatib Ali, aliyezama wakati akirudi kuvua majongoo katika Bahari ya Bumbwini Kiongwe, Wilaya ya Kaskazini B, Unguja.

Wananchi walioshuhudia tukio hilo walisema mvuvi huyo alikuwa amefuatana na wenzake wanne akiwamo baba yake mzazi, Khatib Ali Makame (50), Juma Khatib Ali, Ali Haji Ali na Mjumbe Kiongwe Mjumbe, wote wakazi wa Kiongwe Bumbwini.

Walisema baada ya kushuka mashua waliokuwa wanarudi nayo kuvua, walikuwa wanatembea kwa miguu katika maeneo ya maji madogo, lakini marehemu aliteleza na kuingia kwenye shimo ambalo linakisiwa kuwa na ukubwa usiopungua mita tano kwa ghafla na kwamba hawakuweza kujua kaingia wapi kutokana na kuwa naye mbali.

Kaimu Mkuu Kamandi ya Kaskazini KMKM, Luteni Kamanda Khamis Iddi Juma, alisema Kikosi cha KMKM na Zimamoto vilifika eneo la tukio baada ya kupokea taarifa hizo na kuanza utafutaji wa mtu huyo, lakini hawakufanikiwa kuuona mwili kutokana na maji kujaa na kuwabidi kuahirisha kazi hiyo.

Alisema sababu nyingine iliyokwamisha uokoaji ni kukosa ushirikiano kutoka kwa wananchi wa kijiji.

Alisema uokoaji ulikamilika baada ya askari wa uzamiaji wa vikosi hivyo kuendelea kumtafuta mtu huyo na kuifanikiwa kumwona akiwa ameshafariki majira ya saa 3.30 asubuhi jana.

Aidha, aliwataka wananchi wa kijiji hicho na maeneo mengine kutoa taarifa haraka na ushirikiano kwa vyombo vya ulinzi na usalama wakati yanapotokea majanga ya kijamii ili kurahisisha kazi kwa watendaji au waokoaji katika matukio hayo.

Akizungumza katika eneo la tukio la uokozi, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Bumbwini, Mtumwa Peya Yussuf, alisema amepokea taarifa hizo kwa masikitiko kwa sababu haijapita miezi miwili tangu kutokea kwa ajali kama hiyo katika eneo hilo.

Alivipongeza vikosi hivyo kwa juhudi kubwa wanazochukua za kusaidia wananchi katika majanga mbalimbali bila kujali hali yoyote.

Aliwataka wananchi kuwa makini wanapoenda kufanya shughuli zao za uvuvi katika kipindi hiki ambacho hali ya hewa sio rafiki na matukio kama hayo kuwa mengi.

## China yaisaidia Z'bar miradi maendeleo ya Sh. bilioni 18

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imetiliana saini na serikali ya China msaada kwa ajili ya kusaidia miradi ya maendeleo ya Zanzibar wenye gharama Sh. bilioni 18.

Utiaji saini huo umefanyika jana Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Vuga.

Kwa upande wa Zanzibar, Waziri wa Fedha na Mipango Jamal Kassim Ali, alitia saini mkataba wa msaada huo na kwa upande wa China umewakilisha na Balozi mdogo wa nchi hiyo, anayefanyia kazi zake Zanzibar, Zhang Zhisheng.

Baada ya kusainiwa kwa mkataba huo Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Jamal Kassim Ali, alisema kupatikana kwa msaada huo wa kifedha utasaidia katika miradi ya maendeleo ya jamii na kupunguza kero za wananchi.

Alisema msaada huo utatumika kwa malengo ya kuwatatulia wananchi changamoto zinazowakabili hasa za miradi ambayo Rais aliahidi katika kipindi cha kampeni.

Alisema kila mtu anafahamu kuwa serikali ya awamu ya nane imelenga kuboresha mambo muhimu ili kuwaondolea mwananchi usumbufu ikiwamo majisafi na salama, kuboresha elimu na uchumi.

Alisema msaada huo haukulenga sehemu maalum wala mkataba wa makubaliano haukulazimisha sehemu gani ila kwa upande wa Zanzibar utalenga katika miradi ya maendeleo ya wananchi.

Waziri Jamal alisema kuwa Serikali ya China imekuwa ikiunga mkono jitihada zinazofanywa na Serikali ya Zanzibar hasa za kuboreshaji wa uchumi.

Alisema kuwa fedha hizo zote zitaanza kufanyiwa kazi katika miradi ambayo itakua na tija zaidi kwa wananchi.

Alisema hivi sasa serikali ina hamu ya kutumia uchumi wa bluu kwa maendeleo ya wananchi wake na ukuaji wa uchumi.

Naye Balozi Mdogo wa China, alisema mataifa mbalimbali wanafahamu kuwa Zanzibar na China ni marafiki wa kihistoria na ni washiriki wakubwa wa maendeleo ya Tanzania hasa kwa upande wa Zanzibar.

Alisema Serikali ya China itaendelea kutoa misaada yake kwa Zanzibar katika miradi muhimu inayolenga wananchi kupata maendeleo yao hasa kuondokana na umaskini.

# TAKUKURU yaokoa mil. 20/- za mwalimu mikopo umiza

**Na Gurian Adolf, KATAVI**

TASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Katavi imeokoa cha Sh. milioni 20 za mwalimu mstaafu, George Kamalunde, alizokopa mikopo umiza.

Deni hilo lilimsababishia ugonjwa wa kiharusi, baada ya kufikia kiwango hicho.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani Katavi, Cristofa Nakua, alisema taasisi hiyo iliokoa fedha hizo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa Catherine Mlenga, mke wa mwalimu huyo mstaafu.

Alisema ofisi yake ilipokea taarifa kutoka kwa Catherine kuwa mumewe amedhulumiwa na mfanyabiashara wa mikopo umiza Sh. milioni 20 katika fedha zake za kustaafu.

Nakua alisema baada ya mwalimu huyo kustaafu, fedha za mafao yake zilichelewa kutoka, kitendo kilichosababisha mwalimu huyo kwenda kwa mfanyabiashara wa mikopo umiza na kukopa shilingi milioni 10 kisha akamkabidhi kadi yake ya ATM na namba ya siri.

Baada ya muda, fedha za kustaafu Kamalunde zilitoka na ndipo mfanyabiashara huyo alipochukua shilingi milioni 25, na baada ya kugundua kuwa fedha zote hizo zimechukuliwa, aliugua ghafla na kupata ugonjwa wa kiharusi.

Alisema baada ya uchunguzi ilibainika fedha alizozichukua mtuhumiwa hazina maelezo ya kutosheleza, hivyo aliahidi kurudisha shilingi milioni 20, ndipo akazikabidhi na mlalamikaji amekabidhiwa fedha zake.

Hata hivyo ofisi ya TAKUKURU mkoani Katavi imetoa angalizo kwa wastaafu wa mkoa huo kuwa kama wana shida na wanahitaji kukopa fedha, ni vizuri wakakopa kwenye benki au tasisi za fedha zinazotambulika, kwani huko ndiyo watakuwa salama tofauti na mikopo umiza.



Mbunge wa Jimbo la Ludewa, mkoani Njombe, Joseph Kamonga, akishiriki kupata kinywaji aina ya ulanzi na wananchi wa kijiji cha Shaurimoyo, kata ya Lugarawa, alipotembelea mradi wa chuma wa Liganga hivi karibuni, huku akihamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Waziri: Andikeni wosia

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba, amewataka viongozi wa dini nchini, kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuandika wosia kwa lengo la kupunguza migogoro ya familia.

Dk. Nchemba alitoa rai hiyo jana mkoani Dar es Salaam alipofungua semina ya viongozi wa dini na Wakala wa Ufilisi, Usajili na Udhamini (RITA) kwa lengo la kujadili masuala mbalimbali ikiwamo Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inayotakiwa kufanyiwa marekebisho, masuala ya mirathi na tatizo la ndoa nyingi kuvunjika.

Alisema kumekuwapo na kesi nyingi na malalamiko mengi ya wanawake na watoto kudhulumiwa mali kwa sababu watu wao hawakuacha nakala ya mirathi.

Alisema kuwa tatizo lipo kwa watu kuogopa kuandika wosia, hivyo ni vyema jina likabadilishwa na kuwa kitabu kikuu cha kumbukumbu za familia.

Waziri huyo alisema kutokana na uoga huo, kumekuwapo na ongezeko la matukio mengi ya warithi halali wa mali kurithiwa mali za wazazi wao.

Alisema hata wanaoaminiwa na familia na kuteuliwa kuwa wasimamizi wa mirathi, huwa wanaamini wao ndiyo warithi wa mirathi.

"Sasa kwa sababu viongozi wa dini tupo na jamii kule, tuliona pamoja na kuwa tuna sheria tutajadiliana, mtusaidie kutoa elimu kwa jamii ni ni namna gani watu wetu watarasimisha vitu vyao walivyonavyo kwa watu wao wa karibu," alisema.

Dk. Nchemba alisema kuna watu wanafanya baishara kubwa kwa kushirikiana, lakini hawajaandikisha popote na inapotokea mmoja kafariki, aliyebaki na mali za marehemu anadhulumu ndugu.

"Waelezeni warasimishe na hata sisi turasimishe taasisi zetu, wakati mwingine utasikia huu msikiti tulimwazimisha baba yako au hili kanisa tulimwazimisha tu baba yako eneo. Kama mkiweka maandishi haya, migogoro haitatokea," alifafanua.

Alisema matokeo ya kutorasimisha mali ni mahakama kulaumiwa kuwa imekula rushwa ilhali inatenda haki kulingana na maandishi yanayotokana na kumbukumbu zilizowekwa.

"Wanaodhuliwa mali kwa sababu ya ndugu zao hawakuandika mirathi, walio wema humwachia Mungu na wasiyo wema wanachukua sheria mkononi zinazoleta madhara makubwa kwa jamii," alionya. Alisema suala lingine la kujadili ni kuhusu Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 na namna itakavyowafaa Watanzania wote wenye dini na wasio nazo kabla ya kupelekwa bungeni kubadilishwa.

Pia, aliwataka viongozi wa dini kuwahamishia wananchi kujisajili katika matukio ya msingi yanayotolewa na RITA.

"Kuna mambo tunalenga kuyapata kutoka kwenu, mtuambie nyie mnayaonaje mkiwa kama watunga sera. Mnapochangia msichangie kwa hisia bali mchangie kama watunga sheria au kwa sababu kwenye haya haya masuala yanayohusu ndoa ukiigusa mapana yake yanaenda mbali sana," alisema.

Mwalikishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, ambaye ni Mkurugenzi wa Huduma za Sheria kwa Umma, Griffin Mwakapeje, alisema semina hiyo pia wanapokea maoni ya marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 kifungu cha 12 na 17 ambazo zinaonekana kuathiri watoto wa kike.

Alisema semina hiyo itawapa mwelekeo ambao utawapa mwongozo wa kwenda bungeni kwa lengo la kufanya marekebisho ya Sheria ya Ndoa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa RITA, Emmy Hudson, alisema lengo la semina hiyo ni kuwashirikisha na kuwapa elimu kuhusu huduma hizo na watawapitisha katika mabadiliko yaliyofanyika kisheria katika huduma wanazotoa.

Alizikumbusha taasisi za dini zinazomiliki mali, wanapaswa kuwa na bodi ya udhamini yenye wajibu wa kusimamia mali hizo kwa mujibu wa sheria.

## Mshindi Bonge la Mpango azoa pikipiki miguu mitatu

**Na Lulu George, TANGA**

BENKI ya NMB kupitia kampeni yake ya Bonge la Mpango imekabidhi zawadi ya pikipiki ya miguu mitatu aina ya Lifan kwa mshindi wa droo ya pili ya kampeni hiyo, Yusuph Kyando mkazi wa Mombo Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga.

Pikipiki hiyo inagharimu shilingi milioni 4.4 ambapo tangu kuanza kwa kampeni hiyo Februari, mwaka huu, zawadi zinazogharimu zaidi ya shilingi milioni 35.2 zimetolewa ikiwamo fedha taslimu na pikipiki sita za miguu mitatu aina ya Lifan.

Akizungumza wakati wa kukabidhi zawadi hiyo jana, Meneja wa NMB Kanda ya Kaskazini, Aikansia Muro, alisema zaidi ya shilingi milioni 550 zimetengwa kwa ajili ya kampeni hiyo.

Muro alisema kampeni hiyo ni maalum kwa ajili ya kurejesha faida kwa wateja wa benki hiyo pamoja na kuhamasisha utamaduni wa kujiwekea akiba kwa Watanzania.

"Bado tumelenga kuendeleza mazuri tuliyoyafanya mwaka 2020 mpaka tukaandika historia kubwa katika tasnia ya kibenki kwa kupata faida kubwa zaidi katika historia ya kibenki nchini, alisema Meneja huyo.

Alisema kupitia kampeni hiyo zawadi zimekuwa zikitolewa kila wiki, mwezi na atatafutwa mshindi mmoja wa jumla atakayejishindia gari mpya aina ya Toyota Fortuner.

Muro alitaja zawadi zinazotolewa kuwa ni fedha taslimu kuanzia shilingi 100,000 mpaka 500,000, pikipiki aina ya miguu mitatu (Guta) aina ya Lifan na gari ya mizigo maarufu kama Kirikuu.

Kwa upande wake mshindi wa Bonge la Mpango Yusuf Kyando alisema amefurahi kupata zawadi hiyo ambayo ataitumia kwa ajili ya kujiongezea kipato.

"Mwanzo mimi nilijua ni maneno tu lakini leo ndiyo nimeamini kuwa ni kweli mimi ni mjasiriamali na zawadi hii imeniongezea kipato cha kukuza mtaji wangu kwa kweli nitaitumia kwa kujikwamua kiuchumi," alisema Kyando. Meneja wa NMB Tawi la Mombo, Hamis Mwaduga, alisema wataendelea kuhamasisha wateja kuweka fedha zao benki ili waweze kunufaika na kampeni hiyo.

Naye Meneja wa NMB Tawi la Madaraka, Tanga, Elizabeth Chawiga, alisema kuwa wamepata furaha kwa mshindi wa droo ya pili ya Bonge la Mpango kutokea katika mkoa wa Tanga.

"Niwaombe wakazi wa Mkoa wa Tanga kuweka akiba kwenye akaunti zao kupitia benki ya NMB, lakini wale ambao hawana akaunti waje wafungue kuna faida kubwa sana kuweka fedha zako benki kiusalama lakini kujipatia nyongeza kama hizi," alisema meneja huyo.

HABARI KIMATAIFA

# Kamala asisitiza usawa, demokrasia kwa wanawake

**New York,** MAREKANI

MAKAMU wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, amesema hali ya wanawake ni hadhi ya demokrasia, akiongeza kwamba Marekani imedhamiria kutekeleza maadili ya kidemokrasia yaliyoko katika Azimio la Haki za Binadamu.

Kamala aliyasema hayo wakati akihutubia Kikao cha 65 cha Kamisheni ya Hali ya Wanawake Duniani (CSW65), mjini New York.

"Eleanor Roosevelt, ambaye aliunda Azimio la Dunia juu ya Haki za Binadamu, aliwahi kusema, Bila usawa, hakutakuwa na demokrasia."

Kwa maneno mengine, hali ya wanawake ni hali ya demokrasia. Kwa upande wetu, Marekani itafanya kazi ya kuboresha yote mawili.

Tumejitolea kutekeleza maadili ya kidemokrasia yaliyoingizwa katika azimio hilo. Na tunaamini kwa dhati kwamba, tunapofanya kazi pamoja kimataifa, tunaweza kufikia maono ndani yake."

Kamala alibainisha kuwa anavutiwa na maendeleo yanayofanywa duniani kote katika suala la wanawake na demokrasia na pia anajivunia.

"Hali ya demokrasia pia inategemea kimsingi uwezeshaji wa wanawake. Sio tu kwa sababu kutengwa kwa wanawake katika kufanya maamuzi ni alama ya demokrasia yenye dosari, lakini kwa sababu ushiriki wa wanawake unaimarisha demokrasia.

Na hiyo ni kweli kila mahali. Nikiangalia duniani kote, nimeongozwa na maendeleo ambayo yanafanywa. Na ninajivunia kutoa taarifa kwamba, wakati Marekani bado ina kazi ya kufanya, sisi pia, tunapiga hatua na kwamba wanawake wanaimarisha demokrasia yetu kila siku."

Kikao hicho kinachoendelea nchini humo, kinaipa dunia fursa ya kujadili ushiriki kamili wa wanawake na ufanisi na maamuzi katika maisha ya umma, pamoja na kuondoa ukatili, kwa ajili ya kufikia usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake na wasichana wote.

**UN**



Mwanamke wa Kipalestina, Labiba Abdullah akilima kwenye shamba lake katika kijiji cha Deir Ballut karibu na mji wa Ukingo wa Magharibi wa Salfit, jana. **PICHA: XINHUA**

# Shambulio laua 58 Niger

**Tillabéri,** NIGER

WATU 58 wameuawa nchini Niger, baada ya shambulio lililotokea katika mpaka wa Mali, mamlaka imesema.

Wanaume wenye silaha walikuwa kwenye magari manne wakifyatua risasi karibu na soko katika eneo la Tillabéri.

Hakuna kundi la kigaidi lililodai kuhusika na shambulio hilo ambalo lilitokea Jumatatu.

Hata hivyo hivi karibuni kulikuwa na kampeni za jihadi wawili Niger, mmoja kutoka eneo la Magharibi karibu na Mali na Burkina Faso na mwingine kutoka Kusini Mashariki katika mpaka wa Nigeria.

Katika taarifa iliyosomwa kwa umma katika runinga, serikali ya Niger ilisema, kundi la wapiganaji hao bado halijafahamika na hata gari lililokuwa limewabeba.

"Idadi ya waliokufa imefikia 58, mmoja amejeruhiwa, magari mawili au zaidi kuteketezwa na vitu vingine kuharibiwa katika shambulio hilo," taarifa hiyo ilisema.

Serikali pia ilitangaza siku tatu za maombolezo kitaifa, kuanzia leo jana, kufuatia tukio hilo.

**BBC**

## Maisha jela kutekeleza uasi

**Kinshasa,** DRC

LAURENT Nsubu Katende, kiongozi wa kimila alikuwa mmoja wa viongozi wa wanamgambo wanaohusishwa na uasi wa kundi la watu wenye silaha wa Kamuina Nsapu.

Kundi hilo la waasi lilikabiliana na vikosi vya serikali kati ya mwaka 2016 na 2019.

Laurent Nsubu Katende na wanamgambo wake walishutumiwa kwa kufanya uhalifu dhidi ya raia katika mkoa wa Kasaï Central, mwanzoni mwa mwaka wa 2017.

Hukumu hiyo ilitolewa na mahakama ya kijeshi ya Kananga.

Laurent Nsubu Katende alihukumiwa kwa uhalifu wa kivita kwa mauaji, mateso, ukeketaji, ubakaji, uporaji wakati wa mashambulizi katika vijiji vya jimbo la Kazumba mwanzoni mwa mwaka 2017.

Hii ni hukumu ya kwanza katika mzozo kati ya wanamgambo na vikosi vya serikali, kulingana na Shirika lisilo la kiserikali la Trial International, machafuko yalisababisha vifo vya zaidi ya watu 3,000.

**RFI**

## Sarkozy kizimbani shtaka la pili

**Paris,** UFARANSA

RAIS wa zamani wa Ufaransa, Nicolas Sarkozy, jana alipandishwa kizimbani kwa madai ya ufadhili usio halali wa kampeni yake ya kuwania urais mwaka 2012.

Katika kesi hiyo ya pili dhidi yake, Sarkozy alishtakiwa kwa kuzidisha matumizi ya fedha za kampeni kwa euro milioni 20, kuliko inavyotakiwa kisheria.

Rais huyo wa zamani hatarajiwi kufika mahakamani.

Iwapo atatiwa hatiani atahukumiwa kifungo cha hadi mwaka mmoja jela na faini ya euro 3,750.

Kesi hiyo imefanyika wiki kadhaa baada ya Sarkozy kuhukumiwa kifungo cha miaka mitatu jela, Machi Mosi, mwaka huu.

Awali alipatikana na makosa ya rushwa na matumizi mabaya ya madaraka kushawishi uchunguzi wa masuala yake ya kisiasa kuhusiana na ushindi wake katika uchaguzi wa mwaka 2007.

Sarkozy alikata rufani dhidi ya hukumu hiyo, iliyofuta matumaini ya kugombea tena urais wa Ufaransa.

**DW**



# GUARDIOLA

## AIPANIA LIGI YA MABINGWA ULAYA

**BUDAPEST, Hungary**

PEP Guardiola haamini makovu yaliyopita ya kushindwa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya yaiathiri timu yake ya Manchester City baada ya kufuzu robo fainali.

Mabao mawili kutoka kwa Ilkay Gundogan na Kevin De Bruyne yaliwapa ushindi vinara hao wa Ligi Kuu England dhidi ya Borussia Monchengladbach hapa Budapest, na kuondoka na ushindi wa uwiano wa 4-0, Jumanne.

Hiyo ina maana City wamerudi kwenye hatua hiyo katika mashindano hayo ambapo walikuwa wakitolewa kwa kila msimu kwa misimu mitatu iliyopita, lakini Guardiola hafikirii vichapo walivyovipata dhidi ya Liverpool, Tottenham na Lyon vitawaathiri.

"Kwa misimu iliyopita sikuona timu ambayo haikutaka kufuzu hatua inayofuata. Mara zote tunataka kusonga mbele," alisema akiiambia BT Sport.

"Timu nane bora Ulaya, mara zote ubora ni mkubwa na inakuwa ngumu zaidi kila hatua unayofikia.

"Matumaini yangu timu inaweza kuendelea kuwa kwenye kiwango hiki na tunaweza kushindana, na hasa kwa kucheza mechi nzuri.

"Wakati unaposonga mbele, mara zote naamini hivyo kwa sababu unastahili. Unatakiwa kucheza mechi nzuri.

"Kilichotokea nyuma ni cha nyuma. Kwenye robo fainali, mchezo mmoja mbaya unakufanya uwe na wakati mgunu na kuadhibiwa.

## GUENDOUZI AJIPANGA KURUDI ARSENAL

**BERLIN, Ujerumani**

MATTEO Guendouzi amesisitiza maisha yake ndani ya Arsenal hayajafika mwisho na anataka kupambana kurudi kwenye mipango ya Mikel Arteta msimu ujao.

Guendouzi mwenye umri wa miaka 21, amekuwa na Hertha Berlin tangu Oktoba, mwaka jana ambapo amecheza mechi 19 kwa klabu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani maarufu Bundesliga.

Kiungo huyo wa Ufaransa alikuwa anaanza mara kwa mara katika kikosi cha washikabunduki wakati kikiwa chini ya kocha, Unai Emery, lakini alishindwa kupata nafasi katika wiki za kwanza chini ya Arteta na hivyo akaondoka kwa muda.

Wakati alipoulizwa kama maisha yake ya soka ndani ya Arsenal yamefikia mwisho kutokana na kutokuwa na uhusiano mzuri na Arteta, Guendouzi alijibu kwa kujiamini.

"Hapana, hapana kabisa," alisema akinukuliwa na jarida la France Football.

"Kwa sasa akili yangu kwa msimu huu ipo hapa Hertha Berlin. Halafu tutaangalia cha kufanya na wakala wangu na watu wa klabu kukaa nao chini na kujadiliana kuhusu majaliwa yangu. Mimi bado ni mchezaji wa Arsenal."


Guendouzi alijiunga na Arsenal akitokea Lorient mwaka 2018 na amecheza mechi 57 za Ligi Kuu England kwa washikabunduki hao, akitoa pasi moja ya mwisho huku akiwa hajafunga bao katika mashindano hayo.

# Felix akataa kugombana na Simeone

**MADRID, Hispania**

NYOTA wa Atletico Madrid, Joao Felix amekanusha kuwa ana matatizo na kocha wake, Diego Simeone.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno, ambaye hajawa kwenye kiwango bora hali iliyosababisha Simeone kuhoji mchango wake pale katika dimba la Wanda, ingawa baadaye alikanusha na kusema alinukuliwa vibaya. Felix mwenye umri wa miaka 21, amebainisha kwamba, hana matatizo yoyote na kocha wake.



"Ninafurahi hapa, familia yangu pia. Kuna nyakati nzuri na zile ambazo sio nzuri kila mahali," alisema akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Chelsea jana Jumatano.

"Bila mapenzi na kipaji huwezi kufanikiwa. Wachezaji wengi wenye vipaji wasingeweza kufikia walipo kwa sababu ya kutokuwa na mapenzi na sitaki hiyo kutokea kwangu."

"Uhusiano wangu na Simeone ni mzuri sana. Yeye anajaribu kunisaidia kila wakati. Tuko hapa kusaidiana."




## TUCHEL AKANUSHA WERNER KUONDOKA CHELSEA

**LONDON, England**

KOCHA Thomas Tuchel amecheka uvumi juu ya mustakabali wa Timo Werner pale Chelsea, akiwataka waandishi wa habari "kusoma kitabu" badala ya uvumi wa uhamisho.

Werner anakabiliwa na msimu mgumu wa kwanza pale Chelsea baada ya kutua hapo akitokea RB Leipzig msimu uliopita.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani amefunga bao moja tu la Ligi Kuu England na mwaka 2021 na hajacheka na nyavu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu mechi ya hatua ya makundi dhidi ya Rennes, Novemba, mwaka jana.

Hali hiyo imesababisha ripoti Werner hana furaha pale Stamford Bridge na Tuchel alipoulizwa katika mkutano na waandishi kama nyota huyo mwenye umri wa miaka 25 anataka kurudi Ujerumani, alitoa majibu tofauti.

"Acha kusoma, acha kusoma, unasoma nini uvumi? Soma kitabu," alijibu Kocha huyo juu ya ripoti za kutokuwa na furaha kwa Werner.


"Kwa Timo, nadhani hana sababu sasa ya kuchanganyikiwa kwa sababu alikuwa na mechi ya kushangaza dhidi ya Liverpool, labda mechi yake bora tangu nilipofika," aliongeza.

## IBRAHIMOVIC AITWA KIKOSI CHA SWEDEN

**STOCKHOLM, Sweden**

ZLATAN Ibrahimovic ameitwa katika kikosi cha Timu ya Taifa ya Sweden kwa ajili ya michezo ya kufuzu Kombe la Dunia mwaka 2022.

Ibrahimovic hajaichezea timu hiyo tangu alipotangaza kustaafu kucheza mechi za kimataifa mwaka 2016, lakini amehusishwa tena katika kikosi cha kocha, Janne Andersson.



Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 39 atajiunga na kikosi cha Sweden mwishoni mwa mwezi huu kwa ajili ya kuanza safari ya kuelekea Qatar mwaka 2022 na Andersson amefurahi kumkaribisha tena mfungaji huyo bora wa muda wote wa Sweden.

Alipoulizwa ni kwa nini Ibrahimovic atakileta katika timu baada ya kutangaza kikosi chake kipya Jumanne, Andersson aliwaambia waandishi wa habari:

"Kabla ya yote kwanza, ni mchezaji mzuri na bora kabisa kuwa katika timu ya Sweden.

"Ni kweli inafurahisha kuona kwamba anataka kurejea tena.

"Kwa kuongeza ni nini anaweza kuchangia uwanjani, ana uzoefu mzuri na anaweza kuchangia mengi kwa wachezaji ndani ya timu."

# RONALDO
## ANAWAZA KOMBE LA DUNIA TU

**LISBON, Ureno**

MAJALIWA ya Cristiano Ronaldo kwa klabu yake bado hayajulikani, lakini kocha wa Timu ya Taifa ya Ureno, Fernando Santos amesisitiza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36 ndoto yake ni kucheza na kushinda taji la Kombe la Dunia.

Ronaldo amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka Juventus mwishoni mwa msimu huu, huku kukiwa na uvumi wa kutakiwa kwenye Ligi Kuu Marekani na uwezekano wa kurudi Real Madrid.

Wakati uvumi huo ukizidi kusambaa, Santos amejitokeza na kufafanua kwamba, mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or akili yake ni kucheza na kushinda Kombe la Dunia.

"(Cristiano) ana ndoto kubwa, ndio ninayoijua," alisema Santos.

"Ndoto yake kubwa ni kucheza kwenye Kombe la Dunia na kushinda taji hilo. "Hilo ndilo lengo lake kubwa, mengine yote yapo nje kabisa ya timu ya taifa na yeye mwenyewe."

Ronaldo amecheza katika michuano minne ya Kombe la Dunia, huku nafasi bora zaidi kwake ni wakati Ureno ilipomaliza nafasi ya nne mwaka 2006 nchini Ujerumani, huku wakiwa wametolewa hatua ya 16 kwenye michuano ya mwaka 2010 na 2018.

Ureno ilimaliza nafasi ya tatu kwenye Kombe la Dunia mwaka 1966 kabla ya kushindwa kufuzu kwenye michuano hiyo kwa kipindi cha miaka 20.

Walishinda Kombe la Euro mwaka 2016 huku Ronaldo akifunga mabao matatu, ingawa aliumia dakika za mwanzo tu kwenye fainali.

Ureno itaanza kampeni ya kufuzu kwa Kombe la Dunia baadaye mwezi huu dhidi ya Azerbaijan, Serbia na Luxembourg.

## KWA UFUPI

### MILENKOVIC SOKONI

MANCHESTER United imeanza mazungumzo na wakala wa mlinzi wa Fiorentina, Nikola Milenkovic mwenye umri wa miaka 23, raia wa Serbia. (**Calciomercato - in Italian**)

### LEBRON AINGIA LIVERPOOL

NYOTA wa mpira wa kikapuni nchini Marekani, NBA, LeBron James amekuwa patina wa Kampuni ya Fenway Sports Group, ambayo inaimiliki Liverpool - klabu ambayo alikuwa na hisa nayo tangu mwaka 2011. (**Boston Globe, via Liverpool Echo**)

### BERGE ANUKIA ANFIELD

LIVERPOOL inafikiria uhamisho wa kiungo wa Norway, Sander Berge mwenye umri wa miaka 23 kutoka Sheffield United. (**Eurosport**)

### RONALDO KURUDI UNITED

MSHAMBULIAJI wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, inaonekana anaweza kujiunga na Manchester United kuliko kurudi Real Madrid kama ataondoka Juventus kipindi cha majira ya joto. (**Tuttosport**)

### ABRAMOVICH VS HAALAND

MMILIKI wa Chelsea, Roman Abramovich anataka kumsajili fowadi wa Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20, kutoka Borussia Dortmund. (**Star**)

### GONCALVES ANUKIA UNITED

WINGA wa Sporting Lisbon na Timu ya Taifa ya Ureno chini ya umri wa miaka 21, Pedro Goncalves anawaniwa na Manchester United kwa kuwa gharama yake ni nafuu kuliko Jadon Sancho mwenye miaka 20 kutoka Borussia Dortmund. (**Telegraphsubscriptionrquired**)

### KOUNDE NJIA MOJA

MANCHESTER United imefanikiwa kuishawishi Sevilla kushusha bei ya mlinzi wake, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 22 hadi kufikia pauni milioni 50. (**Sun**)

### SPURS YAMTAKA SANCHEZ

KLABU ya Tottenham Hotspur inamwania nyota wa kimataifa wa Colombia, Davinson Sanchez mwenye umri wa miaka 24. (**Football Insider**)

### CHELSEA, ATLETICO VITANI

CHELSEA imehusishwa na kutaka kumsajili kiungo wa Palmeiras mwenye umri wa miaka 20 raia wa Brazil, Gabriel Menino, ambaye pia anawaniwa na Atletico Madrid. (**UOL, via Sport Witness**)

### SCHONLAU AWINDWA

KLABU ya Norwich City inahusishwa na mpango wa kuwania kumsajili mlinzi wa kati wa Ujerumani, Sebastian Schonlau mwenye umri wa miaka 26. (**Westfalen Blatt, via Eastern Daily Press**)

### GUENDOUZI MTEGONI

KIUNGO wa Arsenal, Matteo Guendouzi (21), amesema atapambana kuhakikisha anarudi kwenye mipango ya Kocha, Mikel Arteta msimu ujao wakati atakapomaliza kipindi cha cha kucheza kwa mkopo kule Hertha Berlin mwishoni mwa msimu huu. (**France Football**)

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ZIDANE AUTAMANI UBINGWA WA UEFA

●●● Mfaransa huyo asema pia analitaka taji la La Liga na hakuna kinachoshindikana kwa...

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane alijibu "kwanini ishindikane" wakati alipoulizwa kama kikosi chake kinaweza kushinda taji la LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya kuifunga Atalanta kweye mchezo wa pili wa hatua ya 16, Jumanne.

Los Blancos hao walikamilisha ushindi wa uwiano wa mabao 4-1 dhidi ya Waitaliano hao kwa kushinda mabao 3-1 mjini Madrid na kufuzu hatua ya robo fainali kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2017-18.

Kikosi cha Zidane ambacho kipo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa LaLiga kikipitwa pointi sita na vinara Atletico Madrid huku zikisalia mechi 11 msimu huu kuchezwa, watajua mpinzani wao wa robo fainali kwenye droo itakayofanyika Ijumaa.

Madrid ilishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu mfululizo kutoka mwaka 2016 hadi 2018, ingawa walishinda LaLiga mara moja tu kwa kipindi hicho."Hicho ndio tutakachokwenda kujaribu kufanya," alisema Zidane wakati alipoulizwa kama wanaweza kushinda LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Kwanini ishindikane? Hiyo ndio sababu tuko hapa. Tutakwenda kujaribu kufanya hivyo. Ni kazi kubwa, lakini tutajitahidi.

"Tuko imara kwenye mashindano yote na usiku huu tumefurahia hilo, sio tu kwa sababu ya mabao tuliyofunga, lakini kwa sababu ya kiwango tulichoonyesha.

"Ukiwa unafanyia kazi vitu na wachezaji wanatoka uwanjani na ushindi, kwa hakika inakufanya uwe na furaha kubwa, hasa kwa timu inayotaka sana mafanikio."

Kiungo wa Croatia, Luka Modric alitajwa kama nyota wa mchezo huo dhidi ya Atalanta, akitengeneza bao la ufunguzi kwa Karim Benzema, kabla ya Sergio Ramos kufunga la pili kwa mkwaju wa penalti na Marco Asensio kufunga la tatu.

## HABARI MICHEZO

# MABADILIKO KATIBA MPYA YANGA YAELEKEA UKINGONI

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga umesema umepokea na kuridhia rasimu ya mabadiliko ya katiba ambayo inaonyesha muundo mpya wa uendeshaji wa klabu hiyo unaotarajiwa kuanza kutumika baada ya kukamilisha mchakato huo, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Haji Mfikirwa, alisema kikao cha Kamati ya Utendaji ya klabu hiyo kilichofanyika chini ya Mwenyekiti, Mshindo Msolla kimeruhusu mchakato huo kuendelea.

Mfikiriwa alisema mchanganuo wa rasimu hiyo umezingatia mapendekezo mbalimbali kutoka kwa wataalamu wa La Liga na Kamati ya Mabadiliko.

Alisema kwa sasa Kamati ya Utendaji imeruhusu mchakato huo kwenda kwa wadau ambao ni hatua ya mwisho.

"Mchakato huo ni kwenye muundo na tayari mabadiliko yamepitishwa, hivyo kamati ya mabadiliko ya katiba chini ya wakili, Raymond Wawa itakaa mapema wiki ijayo kuyaakisi mabadiliko hayo," alisema Mfikirwa.

Hata hivyo aliongeza Kamati ya Mabadiliko inaendelea na mchakato wa kuboresha baadhi ya vitu ndani katika rasimu hiyo na baada ya hapo kamati ya utendaji itakutana tena wiki ijayo ili kukamilisha zoezi hilo.

"Sasa tunakwenda katika hatua ya mwisho ambayo ni kuwashirikisha wadau kwa maana ya vyombo vya serikali ikiwamo Baraza la Michezo Tanzania (BMT), FCC (Tume ya Ushindani), wizara na wadau wa soka, halafu tutarudi kwa wanachama na mwisho kabisa katika mkutano mkuu ambao ndio ngazi ya mwisho ya kutoa uamuzi," alisema Mfikirwa.

Alisema anaamini baada ya kukamilisha mchakato huo, klabu yao itaanza kujiendesha kwa kufuata muundo mpya ambao wanaamini utawasaidia kuwapelekea kwenye mafanikio.




Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Kenya (Harambee Stars), itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Moi Kasarani jijini Nairobi. **PICHA: MTANDAO**

# Kaseja afunguka, Stars uwanjani

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), inatarajia kucheza mechi ya kirafiki ya marudiano dhidi ya wenyeji Kenya itakayofanyika leo, jijini Nairobi, golikipa mkongwe wa timu hiyo, Juma Kaseja amesema anatarajia makubwa kutoka kwa nyota chipukizi walioko katika timu hiyo.

Kaseja ameliambia gazeti hili endapo wachezaji hao wataendelea kunolewa vizuri, anaamini ndani ya miaka miwili Taifa Stars itakuwa na kikosi imara kwa sababu wameonyesha mwangaza.

Golikipa huyo alisema licha ya kufungwa katika mchezo wao wa kwanza, wachezaji hao walionyesha uwezo mkubwa.

"Wachezaji wachanga walioopo kwenye kikosi cha timu ya Taifa wana uwezo mkubwa ukiangalia kwenye mchezo uliopita kati yetu na Harambee Stars walionyesha juhudi licha ya kuwa tulipoteza mchezo, tutarajie makubwa kutoka kwa nyota hawa," alisema Kaseja.

Golikipa huyo amewataka wachezaji vijana ambao hawajapata nafasi ya kuitwa kwenye kikosi hicho kuongeza juhudi wanapokuwa katika klabu zao, ili wamshawishi kocha mkuu wa timu hiyo ambaye atawapa nafasi.

Pia aliwataka Watanzania kuendelea kuipa ushirikiano timu hiyo, ili ifanye vizuri katika mashindano mbalimbali ya kimataifa wanayoshiriki kwa lengo la kupata matokeo mazuri.

Katika mechi ya kwanza ya kirafiki iliyochezwa mapema wiki hii, Stars iliyoko chini ya Kocha Mkuu, Kim Poulsen ilifungwa mabao 2-1.

## Gulioni FC yalia kukosa utulivu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya timu yake kupokea kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Mchangani katika mechi ya Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, Kocha Msaidizi wa Gulioni FC, Khatibu Juma, ametaja sababu iliyosababisha kupoteza mchezo huo ni wachezaji wake kukosa utulivu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Juma alisema wachezaji wake wanatengeneza nafasi nyingi za kufunga, lakini wanashindwa kuzitumia, hivyo wanaambulia matokeo mabaya baada ya dakika 90.

Kocha huyo alisema pia wachezaji wake wamekuwa wakicheza mpira wa 'kitoto' ambao kila mtu anataka afunge goli hata kama hayupo katika nafasi nzuri jambo linalosababisha kupoteza nafasi hizo.

Aliongeza tayari ameanza kulifanyia kazi tatizo hilo, ili wasiendelee kufanya makosa katika kipindi hiki cha kuelekea mwisho wa msimu na hatimaye kupata matokeo chanya.

Baada ya mchezo huo wa juzi, Gulioni imeendelea kusalia katika nafasi ya saba wakati Mchangani FC wenyewe wako kwenye nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 12.

## Polisi Tanzania kujijenga upya

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, amesema atatumia mapumziko waliyopata kupumzisha miili ya wachezaji wake ili baadaye warejee wakiwa na nguvu mpya ya kupambana na kumaliza vizuri msimu huu wa Ligi Kuu Bara ulioko ukingoni.

Ligi Kuu Bara imesimama kupisha Timu ya Taifa (Taifa Stars), ambayo ina mechi za kirafiki kwa ajili ya kujiandaa na mechi za kufuzu Fainali za Kombe la Mataifa Afrika dhidi ya Equatorial Guinea na Libya. Malale alisema anaamini wiki tatu walizopata zitamsaidia kurekebisha makosa madogo madogo aliyoyabaini katika michezo yao iliyopita na hivyo watarejea wakiwa na 'makali' mapya.

"Siku za mapumziko zitawasaidia wachezaji wangu kuimarika zaidi, lengo langu ni kumaliza msimu tukiwa katika nafasi za juu kwenye msimamo, najua tuko kwenye kipindi kigumu kwa sababu kila timu inahitaji kupata matokeo mazuri," alisema Malale.

Aliongeza mchezaji yoyote ambaye ataonyesha uzembe wa kuacha kufanya mazoezi, hatamhurumia na badala yake atamweka benchi na kuwapa nafasi nyota ambao watakuwa kwenye viwango vya juu.

Michezo
Alhamisi Machi 18, 2021
Nipashe



## ZIDANE AUTAMANI UBINGWA WA UEFA

HABARI UK 22




Winga wa Simba, Luis Miquissone (kulia), akipambana kuwatoka wachezaji wa Al Merreikh katika mechi ya Kundi A ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi. Simba ilishinda mabao 3-0. **PICHA: SSC**

## YANGA, METACHA SASA KIMEELEWEKA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema haitambui taarifa zinazosemwa kuhusiana na golikipa wao chaguo la kwanza, Metacha Mnata na kusisitiza mchezaji huyo bado ni mali ya klabu hiyo na si vinginevyo.

Hivi karibuni Metacha aliwaaga mashabiki wa Yanga kupitia ukurasa wake wa Instagram, kauli ambayo iliamsha mtafaruku ndani ya klabu hiyo, lakini baadaye akafuta ujumbe huo aliouandika mtandaoni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Haji Mfikirwa alisema haelewi ni kwa nini baadhi ya watu wanaandika taarifa ambazo si za kweli na hazijatolewa na uongozi wa klabu hiyo.

Mfikirwa alisema anawataka mashabiki wao wapuuze taarifa hizo zinazoendelea kusambaa kwa sababu Metacha bado ataendelea kuitumikia Yanga kwa uadilifu hadi msimu huu utakapomalizika.

"Unajua sasa hivi mitandao ya kijamii, kila mmoja anaandika anavyotaka yeye ili apate watazamaji wengi. Sisi Yanga hatuna mamlaka ya kuwaingilia, lakini tunawaambia tu waache tabia hiyo, vile vile, tunawaambia wanachama na mashabiki wetu taarifa rasmi na za kuaminikla zinapatikana kwenye mitandao rasmi ya klabu na si kwingineko," alisema kiongozi huyo.

Meneja wa mchezaji huyo, Jemedari Said amedai taarifa zinazoendelea kusambaa hazina afya kwa mchezaji na klabu hiyo na aliweka wazi bado Metacha ana mkataba na Yanga.

# GOMES AFUNGUKA ALIPOISHIKA MERREIKH

●●●Kocha huyo asifia pia kiwango cha washambuliaji wake huku akimtaja Mugalu...

**Na Saada Akida**

BAADA ya timu yake kunusa hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes amesema amefurahishwa na matokeo waliyopata na ushindi huo umetokana na wachezaji wake kuonyesha nidhamu ya hali ya juu katika mchezo huo wa mzunguko wa nne uliochezwa bila ya mashabiki hapa nyumbani.

Simba imefikisha pointi 10 na inahitaji pointi moja kati ya mechi mbili zilizosalia na kujihakikishia kusonga mbele kwenye mashindano hayo, kwa sasa ndio vinara wa Kundi A.

Gomes alisema anawapongeza wachezaji wake kwa kucheza vizuri na kufuata maelekezo kwa sababu mechi hiyo ilikuwa muhimu kupata pointi tatu ambazo zimewasaidia kusogea katika hatua ya mbele.

Alisema nidhamu waliokuwa nayo iliwasaidia kutekeleza majukumu vyema huku akifurahishwa pia namna washambuliaji wake walivyocheza akiwamo, Chris Mugalu ambaye alifuta makosa ya mechi iliyopita ya kukosa penalti ambapo juzi alifunga bao la 'kibabe'.

"Kikosi changu kipo vizuri kila idara, hasa ukiangalia safu ya ushambuliaji iko vizuri sana, Meddie Kagere alionyesha kitu katika mchezo huo licha ya kucheza dakika chache, kuhusu nahodha wetu, John Bocco licha ya kutocheza lakini amekuwa muhimiri na mwenye mchango mkubwa katika ushambuliaji.

"Kuhusu hali ya Joash Onyanga inaendelea vizuri na kwa taarifa ambazo nimepewa na daktari wa timu hajapata majeraha makubwa na nina imani atakuwa vizuri na miongoni mwa wachezaji ambao wataenda katika majukumu ya timu za mataifa yao," alisema Gomes.

Naye Kocha Mkuu wa Al Merreikh, Miodrag Jesic alisema wamepoteza mchezo kutokana na matatizo ambayo wamekutana nayo tangu walipowasili Tanzania ikiwamo kuwakosa nyota wake sita wa kikosi cha kwanza ambao waligundulika kuwa na ugonjwa wa Corona.

Hata hivyo Jesic alisema anakubaliana na matokeo hayo anaamini Simba ilifanikiwa kutumia mapungufu yao kupata ushindi huo mnono wa mabao 3-0.

"Tutajiandaa kuiandikia CAF (Shirikisho la Soka Afrika), barua ya malalamiko kuhusu suala hili la wachezaji wetu sita kutocheza kutokana na corona, tunahisi ni njama tu za wenyeji wetu," alisema kwa kifupi kocha huyo mpya ambaye naye ameanza kwa kupata kichapo.

Wakati huo huo, Simba imeingia mkataba na Kampuni ya Emirates Aluminium Profile kwa ajili ya kudhamini Tuzo ya Mchezaji Bora wa Mashabiki wa klabu hiyo ambayo ilianza kutolewa rasmi hapo jana.

Akizungumza jijini jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara alisema udhamini huo utawapa nafasi mashabiki kuchagua mchezaji kulingana na takwimu zake katika michezo ya mashindano yote ambayo timu hiyo inashiriki.

"Unajua Tuzo za Mo zitakuwapo mwaka huu, na vile vile tutatumia mwanya huo pia kutoa tuzo za mashabiki ambazo zimedhaminiwa na Emirates Aluminium Profile," alisema Manara.

Nyota wa kwanza kuchukua tuzo hiyo ya mashabiki ni kiungo mshambuliaji kutoka Msumbiji, Luis Miquissone ambaye pia alikuwa mchezaji bora wa Ligi ya Mabingwa Afrika katika raundi ya pili na alikabidhiwa zawadi ya Sh. milioni moja.

Ofisa Mahusiano wa Aluminium Emirates Profile, Issa Maeda alisema lengo kuu la kuingia mkataba na Simba ni kwa ajili ya kuitangaza kampuni yao na kushiriki kwenye mafanikio ambayo klabu ya Simba imeyafikia.

"Kuna msemo unasemwa kuwa nionyeshe rafiki yako, tukuambie tabia zako na sisi tunaona tunafanana malengo yetu na Simba ndio maana tumeamua kuingia mkataba nao" alisema Maeda.

Miquissoine aliwashukuru waandaaji na kusema kushinda tuzo hiyo ni chachu kwake lakini pia ni kutokana na mchango wa wachezaji wote wa Simba.

"Nashukuru kwa wachezaji wote kwa kujitoa, hii tuzo ni kwa ajili ya wachezaji wote"alisema nyota huyo wa zamani wa UD Songo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042